Alhamisi Desemba 26, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581902

www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

Nipashe digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0677 020 710 LIKE & FOLLOW US

epaper.ippmedia.com Nipashe MIAKA 30 Nipashe Mwanga wa Jamii www.ippmedia.com

UKURASA WA 8

**Mabehewa** ya mizigo 264 ya SGR yatua



UKURASA WA 8

**2,800** mbaroni Songwe, wengi watuhumiwa kwa ukatili kijinsia



UKURASA WA 15

**Watano** wadakwa na magunia 15 ya bangi



## IBADA ZA KRISMASI:

# Maaskofu wang'ata

• **Walia** na Katiba Mpya, kilichojiri Uchaguzi S/Mitaa, utekaji, mauaji, sumu ya michepuko... *Ukurasa 2, 3, 4, 5, 7, 15 na 17*



Baadhi ya waumini wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Iringa wakiwa katika ibada ya kitaifa ya Krismasi iliyofanyika katika dayosisi hiyo jana. **PICHA: FRANCIS GODWIN**



# Bingwa Dk. Mngumi na darasa la unywaji sahihi maji yasikudhuru

UKURASA 12

**MICHEZO** AHOUA, FEI TOTO, HATARI MAGOLI YA PENALTI BARA UK.23 **MAONI,** UK.6



Makamu wa Rais Dk Philip Mpango na Mkewe Mama Mbonimpaye Mpango wakishiriki Ibada ya Sikukuu ya Krismasi katika Kanisa Katoliki Parokia ya wenyeheri Maria Theresa Ledochowska Kiwanja cha Ndege Dodoma jana. **PICHA: OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# Viongozi wa dini wakemea utekaji, rushwa

**Na Waandishi Wetu**

MAHUBIRI ya mkesha wa Krismasi yametawaliwa na nasaha juu ya kulinda amani na upendo huku viongozi wa dini wakiwataka watanzania kudhibiti na kukemea vitendo vya rushwa, utekaji na uvunjifu wa amani kuelekea Uchaguzi Mkuu wa mwakani.

Akihutubia waamini wakatoliki wakati wa mkesha jana katika Kanisa la Bikira Maria Malikia wa Amani, Askofu wa Kanisa Katoliki Jimbo la Geita, Flaviani Kasala alisema sikukuu ya Krisimasi inatakiwa kutumika na watanzania wote kujirudi kwa kukataa matendo maovu yanayoharibu taswira ya taifa.

Alisema matendo hayo ni pamoja na rushwa kwa kuwa watanzania wanaelekea katika Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani, hivyo wakiendekeza rushwa, hakutapatikana viongozi walio na nia ya dhati ya kulitumikia taifa.

Askofu Kasala alitolea mfano Uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliofanyika mwaka huu nchini, akisisitiza kuwa ulionekana kuwa na dosari nyingi, ikiwamo watu kushawishiwa kwa rushwa. Alisema dosari hizo hazipaswi kujitokeza katika Uchaguzi Mkuu.

"Tusikubali kugawanywa wala kutenganishwa na wanasiasa pale tunapoelekea katika Uchaguzi Mkuu wa 2025 badala yake tudumishe amani, upendo na mshikamano," alisema Askofu Kasala.

Kuhusu matukio ya utekaji, Askofu Kasala alisema ni ishara mbaya kwa taifa linaloaminika kuwa kisiwa cha amani, hivyo kuhimiza vitendo hivyo vidhibitiwe na uchaguzi ufanyike kwa amani na utulivu.

Aliwataka waamini wa kanisa hilo kuhakikisha wanakuwa mstari wa mbele kudumisha amani, upendo, mshikamano na kuheshimiana wakati wote kama maandiko matakatifu yanavyoelekeza.

Alisema kuwa kupitia sikukuu ya Krisimas ya kumbukizi ya kuzaliwa Yesu Kristo, ni vyema kila mmoja akajiuliza na kutafakari na kwenda kutenda mema yanayompendeza Mungu.

Askofu wa Kanisa Katoliki Jimbo la Rulenge Ngara, Severine Niwemugizi, katika salamu zake za Krismasi, alisema sherehe hizo si tu za wakatoliki au madhehebu mengine yanayosherehekea, bali zinamhusu kila mmoja kutokana na imani ya ukombozi iliyozaliwa katika Kristo kwa watu wote.

"Kristo ni nuru inayotuangazia sisi ili na sisi tuiangaze kwa wengine na nuru hiyo inaangazwa kwa wote pamoja na madhehebu mengine kwani yeye hakuwapo kwa wale wanaompenda bali wote kwani alimwaga damu yake ili wote tusamehewe dhambi," alisema Askofu Niwemugizi.

Alisema kuwa katika kujitoa ni lazima kujitoa kwa watu wote, akitolea mfano katika mahubiri kuwa kutoa kwa rafiki tu hakuna ulichokifanya bali kwa wote wenye uhitaji.

Mkoani Mwanza, Paroko Msaidizi wa Kanisa Katoliki la Mtakatifu Karoli Luhanga, Nyegezi Jimbo Kuu la Mwanza, Switbert Massao alisema anapozaliwa Mfalme wa Amani, iko haja kila mtanzania kujiuliza kama kuna amani na kuchukua hatua.

Padri Massao alisema kama taifa watu wamejawa na mawazo mbalimbali ambayo yanadhihirisha kupungua kwa hali ya amani kwa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

"Mtu anatoka nyumbani anabaki anawaza 'nguo zangu nimeziacha kwenye kamba, sijuhi nitazikuta', mwingine anatembea anawaza 'sijui mume/mke kwa sasa yuko wapi na anafanya nini'.

"Huo ni wivu na kutokuaminiana, yote hayo yakiwamo na mambo ya wizi, utekaji na vita yanamfanya mtu kukosa amani kutokana na ulimwengu wa sasa kuwa wa kutisha kwa kila mtu," alisema Padri Massao.

Alisema iko haja kuhakikisha kunakuwa na amani nchini na kwenye familia, akisisitiza kuwa nyumba yenye amani inapata wageni, lakini ili yenye vurugu hakuna mgeni atakayetamani kuisogelea.

"Tuhakikishe tunachukua baraka za kuzaliwa kwa Kristo kwa kuishi na kudumisha amani na upendo kwani Kristo ni wa amani, upendo na baraka," alisema Padri Massao.

Paroko wa Kanisa Katoliki Ngokolo, mjini Shinyanga, Adolf Kamandagu, akihutubia waamini katika Kanisa Kuu la Mama Mwenye Huruma Ngokolo, aliwasisitiza watanzania kuendelea kudumisha amani ya nchi.

Alisema chimbuko la amani ni Yesu Kristo ambaye alizaliwa kwa ajili ya kukomboa ulimwengu ambao ulikuwa umeanguka dhambini, hivyo ni vyema wanadamu wote wakaenzi amani hiyo.

"Yesu amezaliwa awe mbaraka kwetu, na ndiye mfalme wa amani. Tusheherekee sikukuu ya Krismasi kwa amani, tuendelee kuomba baraka katika nchi yetu, na amani iendelee kudumu," alisema Paroko Makandagu.

Pia aliwataka watanzania warudishe uhusiano wao na Mungu wao, na kuacha kutenda mambo maovu, bali wapendane, wasiendekeze chuki, viburi na wasitawaliwe na tamaa za kidunia.

Paroko wa Kanisa Katoliki Parokia ya Yesu Kristo Mchungaji Mwema iliyoko Kata ya Buhanda, Manispaa ya Kigoma Ujiji, Achiles Charukula, alisema si kila ugumu wa maisha unasababishwa na laana kutoka kwa Mungu au wazazi, bali ni mpango wa Mungu katika kumwinua mja wake.

Padri Charukula alisema katika kutilitambua hilo ni vyema waamini wa kanisa hilo pamoja na watanzania wote kumrejea Mungu wakati wote na si kuhangaishwa na matatizo pamoja na mahitaji ya jambo fulani.

"Ukiwa mnyenyekevu na mstahimilivu katika matatizo ni kipimo cha Mungu juu ya uvumilivu wako na wala si laana wala nini, hivyo yeye ndiye atakuhusu upate kile kilicho chema kwa ajili yako," alisema Padri Charukula.

Alisema kipindi kigumu katika maisha kiwe chachu ya kumtafuta Mungu na kujua kusudi lake ndani ya mtu badala ya kulalamika na kwamba katika kipindi hicho utukufu wa Mungu huonekana.

Padri huyo pia alitoa wito kwa wanaume wenye familia kutozikimbia pale maisha yanapobadilika na kuwa magumu badala yake uwe ni wakati ambao watashikamana kama ambavyo Yusufu alishikamana na mkewe Mariam katika kipindi kigumu cha kuzaliwa kwa Yesu Krito mkombozi.

Kiongozi huyo wa kiroho pia aliwataka wanawake wote walio na ujauzito, wautunze kwa kula chakula bora na kufanya mazoezi kwa ajili ya kumtunza mtoto aliye tumboni kwa kuwa hakuna mwanamke anayejua amebeba mtoto mwenye hatima gani.

**MAKAMU WA RAIS**

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango na mkewe, Mama Mbonimpaye Mpango jana waliungana na waumini wa Kanisa Katoliki Parokia ya Mwenyeheri Maria Theresa Ledochowska, Kiwanja cha Ndege, mkoani Dodoma katika ibada ya sikukuu ya Krismasi.

Akitoa salamu za sikukuu ya Krismasi kupitia kwa waumini hao, Makamu wa Rais aliungana na Rais Samia Suluhu Hassan kuwatakia wakristo na wananchi wote heri ya sikukuu ya Krismasi.

Aliwataka watanzania kusherehekea sikukuu kwa amani na utulivu pamoja na kujitoa kusaidia wale wasio na uwezo.

Makamu wa Rais pia alitoa wito kwa watanzania kutumia sikukuu ya Krismasi kutafakari juu ya malezi ya watoto majumbani kwa kuwaepusha na vitendo vya ukatili wanavyopitia.

Alisema ni vyema kutafakari nafasi ya watoto katika taifa kwa kuwapelekea tumaini, amani, upendo na furaha.

Makamu wa Rais pia alitoa rai kwa vyombo vya usalama kusimamia vyema sheria za usalama barabarani ili watanzania washerehekee sikukuu kwa amani.

***Imeandaliwa na Alphonce Kabilondo (GEITA), Daniel Limbe (CHATO), Marco Maduhu (SHINYANGA), Adela Madyane (KIGOMA), Vitus Audax (MWANZA).**

*Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz*

## Shoo alia na 'wapangaji wabaya moyoni'

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

ASKOFU wa Dayosisi ya Kaskazini ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dk. Frederick Shoo (pichani chini) amewataka watanzania kuwaondoa katika moyo aliowaita "wapangaji wabaya", akihadharisha hata ukiwa na mali nyingi na maarifa mengi, kama unao wapangaji hao "ni kazi bure".

Amesema matokeo yake si furaha, ni kuishia kwenye uchungu, kukata tamaa na kuchukiana.

Dk. Shoo alikuwa akizungumza jana katika ibada ya sikukuu ya Krismasi iliyofanyika Kanisa Kuu la Usharika wa Moshi Mjini (Cathedral).

Katika mahubiri yake, Askofu Dk. Shoo alisema: "Toa wapangaji wabaya moyoni mwako, ambao wanamzuia Yesu asiingie na asiwe na nafasi katika maisha yako yote.

"Iwe ni kiburi, iwe ni majivuno, iwe ni uchoyo, iwe ni ubinafsi, iwe ni tabia mbaya za kumchukiza Mungu. Hawa ni wapangaji wabaya umewaweka katika moyo wako.

"Inawezekana hata kukosa imani ya kweli kwa Mungu umwaminie. Mali nyingi, maarifa mengi, kama umeweka wapangaji wabaya inakuwa ni kazi bure. Matokeo yake ni si furaha, ni kuishia kwenye uchungu, kugombana, kukata tamaa na kuchukiana."

Zaidi Askofu Dk. Shoo alionya kuwa pasipo Yesu, hayo yote wanayokumbatia, hatma yake ni uchungu na kuangamia.





Viongozi wa taasisi ya Nyansaho Foundation ya mjini Mugumu wilayani Serengeti mkoani Mara, wakiwa na watoto wanaoishi katika mazingira magumu wa Kituo cha Kanisa Katoliki Bunda, baada ya kuwapa zawadi za Krismasi **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Askofu Amani akemea kuuana na 'michepuko' kwa wanandoa

**Na Waandishi Wetu,** ARUSHA

ASKOFU Mkuu wa Jimbo Kuu Katoliki la Arusha, Isaack Amani amewataka wanandoa kuacha tabia ya kuangamizana kwa kuua kwa kukosa upendo.

Pia amewataka wanandoa kuacha tabia ya kuendekeza michepuko" kwa kuwa kufanya hivyo ni kukosa upendo.

Askofu Amani alikemea hayo jana usiku wakati wa misa ya mkesha wa Sikukuu ya Krimasi iliyofanyika katika Parokia ya Tokeo la Bwana iliyoko Burka, jijini hapa.

Aliwataka wanandoa kuacha visa na ugomvi unaosababisha baadhi yao kuangamizana kwa kutoa roho kwa namna tofauti.

Askofu Amani alisema mojawapo ya sababu za kuangamizana ni kukosa upendo ndani ya ndoa na kuwasababisha kuchepuka, kuamsha hasira na kuchukua hatua za kuuana.

Vilevile, aliwataka watoto kuacha tabia ya kuwahisi wazazi wao kuwa ni wachawi na badala yake kufuata kwa umakini amri za Mungu za kuwapenda wazazi na kuwaheshimu.




"Matokeo ya kukosa upendo, kuchepuka, kuuana, ubinafsi na uchawi ni ukatili wa hali ya juu ambao haujengi kabisa taifa lenye nguvu. Yesu amezaliwa kwa ajili yetu, ameleta upendo wa Mungu tuuishi ili kuleta amani na mapatano miongoni mwetu," alisema.

**"Matokeo ya kukosa upendo, kuchepuka, kuuana, ubinafsi na uchawi ni ukatili wa hali ya juu ambao haujengi kabisa taifa lenye nguvu. Yesu amezaliwa kwa ajili yetu..."**

Vilevile Askofu Amani ameelekeza familia ziepuka kuepuka kuwa vichaka vya kuficha uhalifu na kuumizana ili kuishi maisha ya Yesu Kristo.

Alielekeza hayo jana asubuhi jijini Arusha wakati wa mahuburi ya maadhimisho ya Misa ya Krismasi iliyofanyika katika Kanisa la Mtakatifu Theresia wa Mtoto wa Yesu.

"Familiya inatakiwa kuwa mahali salama pa kustahimili, kujifunza utu, kazi na kuheshimiana na kupeana msamaha, haya ndio mambo ya msingi kitika familia, si kichaka cha kuficha uhalifu na kuumizana," alisema.

Alisema ukatili wa majumbani kwenye familia umeenea kote nchini na dunian, utamaduni wa kufichiana siri kwenye ukoo kisa kutoaibisha na kuogopa kutumia sheria unasababisha kuficha uhalifu na ukatili katika familia.

Alishauri watu kujenga utamaduni wa kutumia vyombo vya sheria kutatua migogoro inayojitokea badala ya kumalizana kiukoo kwa lengo la kuficha uhalifu.

Askofu Amani alisema sikukuu ya Krismasi ni fursa kwa wafanyabiashara na huleta furaha, hivyo itumike vyema kuleta amani.

"Utasikia nyimbo zinaimbwa madukani, vyombo vya usafiri na wafanyabiashara wanapata fursa ya kuuza vitu mbalimbali, hivyo kila mtu anapata furaha. Tuitumie kuendeleza furaha na amani," alisema.

Pia aliwaasa waumini hao kukataa tamaa katika maisha yao, badala yake kila mmoja ahakikishe anaishi kwa haki katika ulimwengu wa sasa.

Alitumia mahubiri hayo kuwaasa vijana wanapojiandaa kwa maisha, wajipe muda wa kujifunza stadi za maisha na hasa kazi wanazohitaji.

"Unakuta kijana anaomba kazi, ukimwuliza 'kazi gani?" anajibu 'yoyote'. Nimwuliza kudeki unaweza 'siwezi', kupika 'siwezi'. Sasa unashindwa kumwelewa. Ninaomba watumie muda kujitafakari si kwenda haraka haraka.

"Hata kwa baadhi ya mabinti unakuta anataka kuingia katika ndoa lakini hajajiandaa kuwa katika ndoa, matokeo yake anaingia katika ndoa inavunjika siku mbili kwa sababu hajajiandaa wala hajajipa muda kujitafakari," alisema.

Askofu huyo pia alisema jamii inapita katika changamoto ya rushwa na Ukimwi ambao unasambaa kwa kasi aliyoita "ya ajabu".

Alisema kwa sasa rushwa imekuwa jambo la lazima, watu hunyimwa haki kwa kukataa kutoa chochote na inaweza kugharimu hata maisha ya mtu kwa kukataa kutoa rushwa.

Kwa upande wa maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (VVU), Askofu Amani alisema yanazidi kusambaa katika jamii kwa sababu ya kujiachia kwa tamaa.

"Hii inasababishwa na marafiki wanaishi kama watu wa ndoa na wachumba wanaishi kama watu wa ndoa. Hii ni tamaa! Neno linatuasa usizifuate tamaa za mwili, bali jizuie na tamaa mbaya, ili tuishi kwa amani na furaha," alionya.

***Imeandaliwa na Daniel Sabuni na Cynthia Mwilolezi**

*Kwa maoni: +255 677 020 701*
*Email: customerrelations@guardian.co.tz*

# Mahubiri Krismasi yabeba ajenda Uchaguzi Mkuu, malezi ya watoto

**Na Mwandishi Wetu**

MAHUBIRI ya mkesha wa Krismas katika mikoa ya Mbeya, Njombe na Manyara yamebeba ajenda ya kuhamasisha kuheshimu demokrasia wakati wa Uchaguzi Mkuu mwakani na malezi bora ya watoto.

Padri wa Parokia ya Mtakatifu Bhakita Inyala Jimbo Kuu Katoliki la Mbeya, Mario Luoga aliwataka wanasiasa kuheshimiana na kuzingatia haki ya kidemokrasia wakati wa uchaguzi ili kuepuka migogoro isiyokuwa na maana.

Alisema amani ya nchi inatakiwa kulindwa wakati wote lakini katika kipindi cha mchakato wa uchaguzi ni cha kufanya maombi kwa kuwa ndicho kipindi ambacho wanasiasa wanaweza kuwavuruga wananchi.

"Wakati utakapofika tutaomba sana haki itendeke kwa watu wote, sisi wakristo tunatakiwa kuliombea taifa ili livuke salama kwenye kipindi hicho, lakini wanasiasa wakitenda haki tunaamini kwamba hakuna kitakachoharibika," alisema Padri Luoga.

Askofu wa Jimbo Katoliki Njombe, Eusabio Kyando ameitaka jamii kuacha kujichukulia sheria mkononi badala yake watunze uhai wao na wa watu wengine.

Askofu Kyando aliyasema hayo jana wakati misa takatifu ya sikukuu ya Krismasi iliyofanyika katika Kanisa la Mtakatifu Joseph Jimbo Katoliki Njombe.

Alisema watu wanaona ni rahisi kupoteza maisha ya watu wengine, jambo ambalo ni dhambi hata mbele ya Mungu kwa kuchukua mamlaka yake ya uumbaji.

"Katika ulimwengu huu ambao mambo mengi yanajitokeza na ni Mungu pekee anayeweza kumchukua mtu na kumrudisha kwake.

"Sisi wanadamu wajibu wetu ni mmoja -- kumshukuru Mungu kwa zawadi ya uhai lakini pia kutunza dhamana ya uhai wako na uhai wa mwingine," alisema Askofu Kyando.

Askofu huyo alisema yapo mambo mengi yanatokea hata wakati mwingine watoto kupotea na kuuawa katika mazingira ambayo hayaeleweki na mengine yanasabishwa na imani za kishirikina.

"Mambo mengine mengi ambayo yanatupelekea kuingia huko ni dhambi. Tunatenda dhambi mbele ya Mwenyezi Mungu na hata kwa sababu yoyote ile, unaweza kuwa nayo, huna ruhusa ya kutoa uhai wa mtu," alisema Askofu Kyando.

Askofu Kyando alisema hata waraka aliotoa Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka kuwa na lishe bora ni wajibu wao kuhakikisha wanatunza mwili.

Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Mtaka, baada ya ibada hiyo alisema kuwa baada ya waraka huo, anatamani ujumbe uwafikie wananchi wote wa mkoa huo.

"Katika mwezi huu wa Desemba kumekuwa na visa vingi sana vya watu wa Njombe kujiua, kupoteza maisha ya wenzao. Kama ulivyosema, hakuna mwenye haki hiyo kwa sababu uhai ni zawadi kutoka kwa Mwenyezi Mungu," alisema Mtaka.

Mkoani Manyara, Askofu wa Kanisa Katoliki Jimbo la Mbulu, Antony Lagwen, ameitaka jamii kuombea amani ya nchi kipindi ambacho wananchi wanajiandaa kwa Uchaguzi Mkuu.

Alitoa rai hiyo jana usiku wakati wa mkesha wa Noeli alipokuwa kwenye misa ya kuzaliwa kwa Yesu Kristo.

Alisema maandalizi ya Uchaguzi Mkuu yanapaswa kufanyika kwa kuzingatia demokrasia na kuchagua viongozi wanaotanguliza maslahi ya wananchi na maendeleo.

Kiongozi huyo wa kiroho aliwataka watu wawe bora katika maisha ya kiroho na kufanya ubunifu wa kuboresha maisha yao kiroho.

Alitumia fursa hiyo kukemea ukatili unaendelea katika jamii, akisisitiza kuepukana nao ili watu wafanye shughuli za maendeleo bila kuwa na maumivu ya miili na mioyo.

***Imeandaliwa na Nebart Msokwa (MBEYA), Elizabeth John (NJOMBE) na Jaliwason Jasson (MBULU).**



Wachuuzi wa mboga wakisubiri wateja katika eneo lao la biashara Mbezi Mwisho Dar es Salaam jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# 'Serikali ifanyie kazi dosari za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa'

**Na Jenifer Gilla**

ASKOFU wa Kanisa la Kiinjili ya Kilutheri Tanzania ( KKKT) Dayosisi ya Iringa, Dk. Blaston Gavile ameitaka serikali kufanyia kazi changamoto zilizojitokeza katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ili zisijitokeze katika Uchaguzi Mkuu unaotarajiwa kufanyika mwakani.

Alisema hayo jana wakati wa ibada ya sikukuu ya Krismasi iliyofanyika Kanisa Kuu la KKKT Usharika wa Iringa.

Alisema changamoto zilizojitokeza katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliofanyika Novemba mwaka huu, zinapaswa kufanyiwa kazi na wahusika wa pande zote ili zisijirudie na uchaguzi ujao uwe wa haki na amani.

Aliwakumbusha watanzania umuhimu wa kuombea Uchaguzi Mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba mwakani ili Mungu awaletee viongozi wenye sifa na wanaohitajika kwa majira na nyakati zilizopo.

Kiongozi huyo wa kiroho aliwasisitiza wananchi kujitokeza kugombea nafasi mbalimbali zitakazokuwapo na kupiga kura kwa kufuata miongozo ya tume.

"Haki na amani vitawale katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 na si vinginevyo," alisema na kupongeza watanzania kwa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliofanyika Novemba mwaka huu, akiamini kuwa kila mmoja alitumia haki yake ya kikatiba kushiriki tukio hilo.

"Wale ambao wamechaguliwa katika nafasi mbalimbali na wale ambao hawajachaguliwa, wote tuungane pamoja kujenga nchi yetu hii," alihimiza.

Askofu huyo alishauri serikali iweke mazingira mazuri kwa wakulima na wafanyabiashara wadogo nchini ili wafanye kazi zao katika mazingira salama, yaliyopangwa na yenye kuwaletea uhakika wa kesho ya maisha yao kwa kuwa wao ndiyo kundi kubwa zaidi nchini.

Alikumbusha serikali kutimiza ahadi ya bima ya afya kwa watu wote ili iwasaidie watanzania ambao wengi hawana uwezo wa kumudu gharama za matibabu kwa ngazi ya mtu mmoja hadi familia kutokana na vipato vyao kuwa vidogo.

Pia alitoa wito kwa serikali kuwasaidia wakulima mbegu za muda mfupi ili kuwapo chakula cha kutosha kwa kuwa kuna dalili kuwa hali ya mvua ya sasa haitokidhi haja ya wakulima wa mazao ya muda mrefu kama ilivyozoeleka.

Askofu Dk. Gavile pia alikemea vitendo vya ukatili vinavyoendelea nchini hasa Iringa ambao ni miongoni mwa mikoa yenye matukio mengi ya ukatili nchini.

Vilevile, alikemea vitendo vinavyoashiria imani ya kishirikina katika jamii, ukiwamo uvunjaji nazi barabarani, ubakaji wa watoto na ulawiti.

**"Haki na amani vitawale katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 na si vinginevyo," alisema na kupongeza watanzania kwa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliofanyika Novemba mwaka huu,...**

"Hivi ni vitendo vya aibu na udhalilishaji kijinsia kwa namna mbalimbali, ni dalili za watu wasio na Mungu, ambao hawajastaarabika, tukemee tabia hizi kwa njia zote kwa sala na mifumo yetu," alihimiza.

Askofu Gavile pia aliwataka watanzania kupunguza muda wa sherehe na starehe ili watumie muda mwingi kufanya kazi kwa bidii ili kujiletea maendeleo.

Alimpomgeza Rais Samia Suluhu Hassan na wasaidizi wake kwa uongozi mzuri na kazi kubwa anazofanya, ukiwamo uwekezaji mkubwa wa miradi kama vile Bwawa la Kuzalisha Umeme la Mwalimu Nyerere, na reli ya kisasa (SGR) na kurudishwa vifurushi vya bima ya afya kwa watoto, maarufu Toto Afya Kadi.

"Niwasihi watanzania wenzangu, tulinde miradi hii na kuitunza ili ije iwanufaishe na watu wa vizazi vijavyo," alisema Askofu Gavile.

Akihubiri katika ibada hiyo, Askofu wa Kanisa Kuu la Kilutheri Anglikana Dayosisi ya Ruaha, Dk. Joseph Mgomi, aliwataka waumini wa kikristo kujifunza kupitia maisha ya wazazi wake Yesu, Mariam na Yusufu tangu Mariam alipopata ujauzito kabla ya kushiriki tendo na mchumba wake.

Alisema kama ingekuwa ni maisha ya kawaida, pengine wawili hao wangetengana lakini kwa kuwa walikuwa wakiisikia sauti ya Mungu na kuitii waliendelea na uhusiano wao mpaka walipomzaa mkombozi wa ulimwengu.

Alisema hata mazingira ya kuzaliwa mtoto yalikuwa magumu kwa kuwa alizaliwa katika zizi la ng'ombe lenye mazingira machafu, lakini ilipaswa kuwa hivyo kwa sababu ni mpango wa Mungu.

Alisema kuna wakati binadamu wanapopitia changamoto, wanajilaumu na kusema kuwa pengine wamemkosea Mungu au anawaonea kwa kuwa wamekosa uaminifu kwake.

Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT), Mchungaji Canon Matonya aliwaomba watanzania kusherehekea sikukuu hiyo kwa furaha na amani na kila mmoja amheshimu mwenzake kwa kuwa ameunbwa na Mungu.

Mgeni Maalumu Jesca Msavatavangu, Mbunge wa Iringa Mjini, aliwashukuru viongozi wa dini kwa kuendelea kuliombea taifa na viongozi wakuu wa serikali, akiwamo Rais Samia.

Aliwakumbusha waumini kutambua dhumuni la wao kuwapo duniani kama Mungu alivyowaelekeza -- kutawala, kuzaliana na kutii.

Aliwakumbusha wanaume nchini kuendelea kuwa viongozi katika familia na jamii kwa ujumla na wanawake wasimame katika nafasi zao kuhakikisha dunia inakuwa njema.

# Askofu: Kama hakuna Katiba Mpya, Uchaguzi Mkuu wa 2025 uahirishwe

## -Ashtuka wananchi kufurahia ajali ya wabunge

**Na Waandishi Wetu,** DODOMA

ASKOFU wa Kanisa la Baptist Tanzania Kanda ya Kati, Antony Mlyashimba, ameshauri kuwa, kama hakutakuwa na Katiba Mpya, Uchaguzi Mkuu wa 2025 uahirishwe ili kuliepusha taifa kuingia katika chuki na visasi.

"Ili kuondoa chuki iliyopo hivi sasa baina ya watanzania, suluhu pekee ni kupatikana kwa Katiba Mpya pamoja na Tume Huru ya Uchaguzi. Hivi sasa kama taifa tumefikia sehemu mbaya sana ambayo watu wanafurahia mabaya yanayowatokea wenzao," ametamka.

Askofu Mlyashimba alitoa kauli hiyo jana wakati wa mahubiri yake ya sikukuu ya Krismasi yaliyofanyika kwenye Kanisa la Baptist Makole, jijini hapa.

"Hivi karibuni kuna taarifa zilizushwa kwenye mitandao ya kijamii kuwa Rais wetu yuko ICU, lakini maoni yaliyokuwa yanatolewa watu wanasema..." alitamka.

Huku akinukuu kauli nzito zisizofaa katika jamii, askofu huyo akaendelea: "Tukio la ajali kwa wabunge lilipotokea, watu walifurahi sana..."

Alifafanua kauli yake kuhusu Uchaguzi Mkuu 2025 kwamba iwapo utafanyika pasipo kuwapo "Katiba Mpya na Tume Huru ya Uchaguzi, serikali inapaswa kuuahirisha hadi mwaka 2026 ili mwaka 2025 utumike kupata mifumo bora ya kusimamia uchaguzi huo."

**ASKOFU ANGLIKANA**

Naye, Askofu wa Kanisa Aglikana Tanzania Dayosisi ya Central Tanganyika, Dk. Dickson Chilongani, akihubiri kwenye ibada ya Krismasi katika Kanisa Kuu la Roho Mtakatifu Dodoma, alishauri Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kuacha matumizi ya nguvu wakati wa ukusanyaji mapato kwa wafanyabiashara.

Alisema TRA wanapaswa kuzingatia ushauri wa Rais Samia Suluhu Hassan wa kuweka mazingira rafiki kwa wafanyabiashara wakati wa ukusanyaji mapato badala ya kutumia nguvu na mabavu.

Vilevile, aliwataka watanzania kuhakikisha kwenye Uchaguzi Mkuu 2025 wanachagua viongozi ambao wataziishi shida zao badala ya watakaosoma kero zao kwenye magazeti na mitandao ya kijamii.

"Tuchague viongozi ambao wanazijua vizuri shida zetu watanzania, siyo wale ambao watasoma shida zetu kwenye magazeti na mitandao ya kijamii," alisema Askofu Dk. Chilongani.

Askofu Msaidizi wa Jimbo Kuu Katoliki la Dodoma, Wilbroad Kibozi, aliwataka wazazi na walezi katika familia kuzingatia suala la kuwalea watoto kwenye maadili mazuri ili kutengeneza viongozi bora wa kitume na serikali.

Askofu Kibozi alisema hayo wakati akitoa mahubiri kwenye mkesha wa sikukuu ya Krismasi uliofanyika katika Kanisa la Mtakatifu Gaspery De Bufalo Parokia ya Makole, jijini hapa.

Alisema msingi mzuri wa malezi ya watoto unaanzia katika familia, hivyo wazazi wanao wajibu wa kuwajengea imani itakayopeleka kuzalisha vijana wenye maadili na misingi bora.

"Ninawakumbusha wazazi jukumu lenu la kulea watoto katika familia. Tunapenda kuona taifa linakuwa na vijana wenye maadili mazuri," alisema Askofu Msaidizi Kibozi.

***Imeandaliwa na Paul Mabeja na Renatha Msungu.**

*Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz*

# KRISMASI PICHANI




Mchungaji wa kanisa la KKKT Usharika wa Muheza Tanga, Elias Majo akiongoza ibada kwa waumini kanisani hapo jana wakati wa sikukuu ya Krismasi. **PICHA: STEVEN WILLIAM**



Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania Dayosisi ya Iringa, Dk Blaston Gavile (kulia) na viongozi mbali mbali wa makanisa wakipokea maandamano nje ya kanisa KKKT usharika wa kanisa kuu wakati wa ibada ya kitaifa ya Krismasi iliyofanyika KKKT Dayosisi ya Iringa jana. **PICHA: FRANCIS GODWIN**



Baadhi ya wachungaji wakiwa na mbunge wa Iringa Mjini, Jesca Msambatavangu wakati wa ibada ya Krismasi iliyofanyika KKKT Dayosisi ya Iringa jana. **PICHA: FRANCIS GODWIN**



Baadhi ya waumini wakiwa katika ibada ya Sikukuu ya Krismasi katika Kanisa Katoliki Parokia ya Mwenyeheri Maria Theresa Ledochowska Kiwanja cha Ndege Dodoma jana. **PICHA: OFISI YA MAKAMU WA RAIS**



Waumini wakiwa katika ibada Krismasi katika Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Usharika wa Muheza mkoani Tanga jana. **PICHA: STEVEN WILLIAM**



Mpiga kinanda wa kwaya ya St. Joseph, Edward Celestin wakati wa ibada ya mkesha wa Krismasi mjini Zanzibar jana. **PICHA: MARTIN KABEMBA**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kero za shule jirani na makaburi sasa zitatuliwe

**WIKI** iliyopita tulikuwa na ripoti maalumu kuhusu Shule ya Msingi Lipumba, wilayani Mbinga, mkoa wa Ruvuma ambayo madarasa yake yamejengwa jirani na makaburi ya kijiji.

Ujirani huo wa madarasa na makaburi, kama ilivyobainika katika uchunguzi wa Nipashe, unawaathiri wanafunzi si tu kisaikolojia, bali pia kukosa baadhi ya vipindi vya masomo kutokana na walimu wao kusitisha ufundishaji na kulazimika kuungana na wanakijiji katika shughuli za maziko.

Si hili tu, shule hiyo yenye wanafunzi 451, inakabiliwa na uhaba wa miundombinu na uchakavu wa miundombinu michache iliyoko shuleni.

Imebainika katika uchunguzi wa Nipashe kuwa shule hiyo ya serikali iliyoanza kutoa huduma miaka 49 iliyopita, ina vyumba saba vya madarasa, vitano vikikabiliwa na uchakavu mkubwa.

Mbali na kuwa na nyufa, sakafu ya madarasa hayo imeshabomoka na mahali pengine pana mashimo; plasta kwenye baadhi ya kuta imebanduka kiasi kwamba unaweza kuhesabu idadi ya matofali ya kuchoma yaliyotumika kujenga madarasa hayo.

Katika moja ya madarasa, kama ilivyobainika katika uchunguzi wa Nipashe, mlango umeshang'oka na kuwekwa pembeni ndani ya darasa hilo; mabati ya paa yana kutu na ishara zote za kuoza.

Idadi hiyo ya wanafunzi 451 kutoka Shule ya Msingi Lipumba, wote wa kijiji cha Lipumba, wana shida nyingine inayohusu vyoo. Viko katika hali mbaya inayokinzana na uhalisia wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 (marejeo ya 2023) na maelekezo mbalimbali, yakiwamo mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ya Machi 2017.

Hali halisi ya kilichoshuhudiwa shuleni Lipumba kina ishara ya kukinzana na miongozo mingi ya kitaifa kielimu, hata kimaendeleo, ikienda mbali kufikia nadharia ya taaluma ya elimu duniani.

Nchini Tanzania kunakopatikana shule ya Lipumba, ndani ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 (marejeo ya 2023), kuna vipengele vinavyogusa mambo muhimu mawili: Elimu ya Kujitegemea iliyoanza mwaka 1967 na Azimio la Musoma la Mwaka 1974.

Elimu ya Kujitegemea inamtaka mwanafunzi, akiwamo wa shuleni Lipumba, kupata elimu hiyo yenye sura ya kuwa na ujuzi, ufahamu na maarifa yanayoendana na mazingira ya kitanzania, pia anawanufaisha nayo watanzania.

Vilevile, mhitimu huyo wa Lipumba atautumia ufahamu aliopata kwa ngazi yake, ukimwezesha kumudu mahitaji yake ya kimazingira na kimaendeleo, mfano katika tahadhari za kiafya, pia shughuli za kilimo.


Katika mtazamo mpana, kwa sasa Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, inaitegemea sekta ya elimu, ambayo karakana yake mojawapo ni shuleni Lipumba, iisaidie katika kuongeza maendeleo ya rasilimaliwatu kwa kutayarisha watanzania mahiri walioelimika ili kuletea taifa maendeleo endelevu na kuliweka kwenye uchumi shindani duniani.

Mazingira ya sasa ya shuleni Lipumba hayasadifu mahali panapohitajika kisera kuzalisha rasimaliwatu inayotajwa katika dira tajwa.

Kuna taarifa kwamba aina fulani ya hatua zinachukuliwa, uongozi wa serikali mkoani Ruvuma katika safu yake ya wilayani Mbinga ukizuru shuleni kujionea kilichoripotiwa na Nipashe. Ni hatua nzuri inayostahili pongezi za awali.

Lakini hii haitoshi. Jibu kuu la wanafunzi na walimu wao shuleni Lipumba ni kutatuliwa adha tajwa zinazoathiri taaluma na ustawi wa kazi kwa kundi zima linaloshughulika na elimu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

Na Mwandishi Wetu

# Tumuunge mkono Rais kwa kampeni nishati safi na nduguye utunzaji miti

**SERIKALI** imekuja na mwarobaini wa kutokomeza ukataji miti ovyo, kwa ajili ya matumizi ya kupika majumbani kwa mkaa na kuni.

Matumizi hayo ya kupikia mkaa na kuni, yamegeuka utamaduni katika jamii maeneo ya mijini na vijijini.

Kwa vijijini, idadi kubwa ya wananchi wanaoishi huko wamekuwa wakitumia kuni kwa matumizi yao ya kila siku kutoka kwenye misitu, baada ya miti kukatwa na kuanguka.

Kwa upande wa mkaa, matumizi yake kwa kiwango kikubwa ni kwa maeneo ya mijini ambako hakuna mashamba ya miti na misitu iliyotengwa mahususi kwa hifadhi za serikali.

Ni ukweli usiopingika kuwa ukataji miti kwa kiwango kikubwa unachagizwa na biashara ya mkaa katika maeneo ya mijini ambako kuna watumiaji wakubwa kwa ajili ya kupikia majumbani.

Watumiaji wengine ni wafanyabiasha wa mahindi ya kuchoma, nyama na wafugaji kuku wa kisasa kwa ajili ya kuweka joto kwenye mabanda yenye vifaranga dhidi ya baridi.

Kutokana na kuendelea kwa kasi ya ukataji miti katika maeneo mbalimbali nchini, serikali nayo imesimama kidete kupinga vitendo hivyo, kwa kuanzisha kampeni mbalimbali na kutunga sheria kali dhidi ya wanaojihusisha na vitendo hivyo.

Mbali na serikali, kumekuwapo na taasisi, kila moja ikijihusisha na uhifadhi na utunzaji mazingira kivyake hususani miti kutokana na tishio la baadhi ya maeneo nchini kugeuka jangwa.

Madhumuni ya taasisi hizo yana lengo la kuisaidia serikali kufanikisha kampeni yake ya kupiga vita ukataji miti ovyo, kwa matumizi ya kupikia majumbani na mbao bila ya kuwa na vibali.

Kampeni hiyo ya serikali, imekuwa ni pamoja kuhimiza 'kata mti panda mti' ili misitu iwe endelevu na uoto wa asili.

Pamoja na kampeni hiyo na nyingine za serikali, taasisi hizo zinatakiwa kuwa na mawasiliano, ili nchi ifanikishe malengo yake kwa manufaa ya wananchi na vizazi vijavyo.

Taasisi hizo zinatakiwa kufanya kazi kama timu moja badala ya kila moja kivyake, vinginenyo zitashindwa kubeba maono yaliyoko kitaifa. La msingi la misitu na uhifadhi wa misitu ambavyo katika jamii imezoeleka kuwa ni mazingira na uhifadhi wa mazingira.

Mazingira yanabeba maana kubwa, wengi maana yao ikiishia kwenye uchafu na usafi katika maeneo wanayoishi.

Serikali ina wajibu wa kuwaagiza maofisa wake wa misitu, waendeshaji wa mashauri mahakamani, mahakimu na viongozi wa serikali za mitaa, vijiji na vitongoji kuwaelimisha wananchi umuhimu wa kutunza miti na kuhifadhi mazingira yao kwa manufaa yao.

Hiyo itaondoa changamoto ya kukosa hewa safi, kudhibiti magonjwa na kufahamu sheria za ulinzi misitu.

Hadi sasa kuna nchi duniani zimefanikiwa kukabiliana na changamoto za kukosa mvua na magonjwa baada ya wananchi wake kupatiwa elimu na kutumia sheria kali dhidi ya ukiukwaji wowote.

Hivyo, Watanzania tuendelee kuhimizana kutunza misitu kwa wafanyabiashara wa mkaa na kuni kubuni biashara mbadala ya kujikimu kwa maisha na familia zao, kwani kutasaidia kufanikisha malengo ya serikali.

Vilevile ni wakati serikali ikadhibiti taasisi zinazoharibu mazingira, kamwe isiziache; ukataji miti na kuzuia kukata miti badala yake zote zifanye kazi moja tu kudhibiti ukataji ovyo.

Kwa upande mwingine, serikali ikazie na wanaopatikana na hatia, waadhibiwe kwa mujibu wa sheria zilizoko, huku wakiwajibishwa kufidia miti wanayokata. Naamini, hatua hiyo itasaidia kudhibiti ukataji miti badala ya kupewa adhabu ya kwenda jela.

Wakati yote yanajiri, kampeni ya matumizi ya nishati safi ya gesi kupikia inayoendelea nchini, itasadia kudhibiti ukataji miti ovyo kwa ajili ya kuni na mkaa.

Kampeni hiyo katika mikoa mbalimbali nchini, itaongeza idadi ya watumiaji gesi kupikia majumbani na sehemu za biashara, kama vile kwa mama na baba lishe.

Utafiti uliofanyika mwaka 2020 unaonesha idadi kubwa ya wananchi wapatao asilimia 63.5 wanatumia kuni kupikia, 26 mkaa na asilimia tano gesi.

Kwa mujibu wa takwimu hizo, nishati safi ya kupikia bado ni changamoto katika jamii, hivyo Rais Samia Suluhu Hassan 'kumtua kuni mwanamke kichwani' iende sambamba na elimu katika jamii kwani italeta mafanikio makubwa nchini.

Mafanikio hayo yanagusa kutokomeza magonjwa yanayosababishwa na hewa ya ukaa yaani chafu kutokana na matumizi ya kuni na mkaa.

Mengine ni kutunza, kuhifadhi misitu na kupata mvua za kutosha nchini na kuokoa muda wakati wa kupika na jamii kufanya shughuli za uzalishaji mali.

HABARI KITAIFA

# Wakulima waonywa kuficha mifugo kupatiwa chanjo

**Na Thobias Mwanakatwe**, DODOMA

NAIBU Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Abdul Mhinte amewaagiza viongozi wa vyama vya wafugaji kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa wakati wa chanjo ya mifugo itakayoanza Januari mwakani ili kuhakikisha wafugaji hawafichi mifugo.

Akizungumza juzi wakati akifunga kikao kazi cha uhamasishaji kampeni ya chanjo kitaifa kilichokuwa kinafanyika jijini Dodoma, Mhinte alisema wafugaji wahakikishe wanatii Sheria ya Magonjwa ya Wanyama ya Mwaka 2003 na Kanuni za Chanjo na Uchanjaji za Mwaka 2020.

"Unakuta mfugaji ana ng'ombe 500 halafu anachanja 100, wengine anawaficha porini. Baadaye zoezi letu linaonekana lina shida, niwaombe viongozi wa vyama vya wafugaji na wafugaji tushirikiane, msifiche mifugo wakati wa uchanjaji," alisema.

Mhinte pia aliwahimiza wafugaji kuendeleza maeneo ya malisho ya mifugo yatakayosaidia kuondoa migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi.

Mkurugenzi wa Idara ya Huduma za Mifugo, Dk. Benezeth Lutege alisema chanjo ya mifugo itakayotolewa awamu hii inazalishwa na Serikali ya Tanzania na imethibitishwa na Mamlaka ya Chakula na Dawa (TMDA), hivyo wafugaji wathamini chanjo zinazozalishwa nchini. "Kampeni yetu itatumia chanjo inayozalishwa na Viwanda vyetu vya ndani, ni chanjo salama na imethibitishwa na TMDA. Pia imepata kibali cha maabara ya Kanda ya Afrika na tumekuwa tukisafirisha hata nje ya nchi," alisema. Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Uendelezaji Maeneo ya Malisho, Gabriel Bura, alisema chanjo ya mifugo inapaswa kwenda sambamba na uzalishaji malisho ili mifugo inapochanjwa iwe imepata chakula kuwezesha chanjo hiyo kufanya kazi.

Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Ufugaji Tija (CHAMAUTA), Ester Moreto, alisema elimu inahitajika kuongeza uelewa kwa wafugaji ili kutokomeza magonjwa ya mifugo na kuongeza thamani ya mazao ya mifugo yanayozalishwa nchini.

"Mimi nina miaka minne ninachanja ng'ombe wangu na hawajawahi kuwa na shida yoyote. Niwaombe wafugaji wenzangu wasifiche mifugo, wachanje wote. Pia serikali itoe elimu na hamasa kwa wafugaji kote nchini," alisema.

Katika awamu ya kwanza ya mpango huo wa chanjo, serikali kupitia wataalamu wa Sekta ya Mifugo na Mamlaka za Serikali za Mitaa inatarajia kuchanja ng'ombe 19,097,223 dhidi ya ugonjwa wa homa ya mapafu ya ng'ombe (CBPP), mbuzi na kondoo 20,900,000 dhidi ya ugonjwa wa sotoka ya mbuzi na kondoo (PPR).

Kuku wa asili 40,000,000 watachanjwa dhidi ya ugonjwa wa mdondo wa kuku (ND) ambapo lengo la serikali ni kutoa chanjo kwa mifugo angalau asilimia 70 ya idadi ya mifugo husika kwa miaka mitano mfululizo.



Mkazi wa jijini Dar es Salaam akisafirisha madumu kwa baiskeli eneo la Ubungo jana, huku yakiwa yamemziba kuona nyuma, kitendo ambacho si salama kwake. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Askofu Malasusa aonya vitendo vya utekaji

**Na Elizabeth Zaya**

MKUU wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Alex Malasusa amesema mwaka huu taifa limepitia wakati mgumu kutokana na matukio ya kutekwa, akisisitiza matukio hayo yasijirudie mwakani.

Dk. Malasusa ambaye pia ni Askofu wa Dayosisi ya Mashariki na Pwani, alitoa kauli hiyo jana wakati akihubiri katika ibada ya sikukuu ya kumbukizi ya kuzaliwa Yesu Kristo katika Kanisa la KKKT Usharika wa Azania Front, jijini Dar es Salaam.

Alisema kuwa tangu azaliwe hajawahi kuona matukio kama hayo ya utekaji nchini kama ilivyotokea mwaka huu.

"Watanzania tumepitia kipindi kigumu sana, hasa mambo ya watu kutekwa. Tangu kuzaliwa kwangu sijawahi kusikia wala kuona watu kutekwa kama ilivyokuwa katika kipindi hiki.

"Juzi nikiwa katika gari, alikuja askofu mmoja akanishika na nilikuwa sijamwona, nilishtuka, ilikuwa kama saa moja hivi jioni, akaniambia 'shhh...!' Ndipo nikamwambia 'vipi askofu?' Yaani lugha ya kutekwa imeleta hofu, hata mtu akikusogelea kukusalimia, unaogopa," alisema.

> **"Tunaomba vitendo hivi viwe mwisho, visijitokeze tena mwaka ujao, wale wenye roho za kuwachukua watu na kuwahangaisha, Mungu ashukughulike nao," alisema Askofu Dk. Malasusa.**

Alisema wanamwomba Mungu vitendo hivyo visijitokeze tena mwaka ujao na mwaka huu iwe mwisho huku akisema kuna haja kwa watanzania kumwomba Mungu ili hali hiyo iishe.

"Tunaomba vitendo hivi viwe mwisho, visijitokeze tena mwaka ujao, wale wenye roho za kuwachukua watu na kuwahangaisha, Mungu ashukughulike nao," alisema Askofu Dk. Malasusa.

"Tuna hofu nyingi katika maisha, hofu ya uchumi, hofu ya ndoa, ndoa nyingi zimeharibiwa na watu wa karibu, ni vyema kumshirikisha Mungu katika ndoa yako badala ya 'mabest man'," alisema.

Akizungumzia Uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliofanyika mwaka huu, Askofu Dk. Malasusa alisema uligubikwa na vitendo vya uvunjifu wa amani na iwapo hali hiyo isipoangaliwa inaweza kujirudia tena katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka kesho.

"Wakati mwingine tumeona kabisa kuna watu ambao hawaipendi amani. Tulipokuwa tunapita kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka huu, nimeona kabisa kuna watu ambao hawapendi amani. Katika uchaguzi huo, niliona kabisa kuna viashiria vya uvunjifu wa amani. "Kama hatutaviangalia katika Uchaguzi Mkuu ujao vinaweza vikajirudia, ni lazima tuombe, kuanzia sisi wapigakura, wale watakaojaribu kupata uongozi, lakini wale wenye mamlaka ya kusimamia uchaguzi ili tupite salama, ninaamini katika mazungumzo kwa ule upungufu ambao unaweza kujitokeza," alisema Mkuu wa KKKT.

ASKOFU RUWA'ICHI

Naye, Askofu Mkuu wa Kanisa Katoliki Jimbo kuu Dar es Salaam, Yuda Thaddeus Ruwa'ichi amezungumzia umuhimu wa watu kuhesabiwa, akifafanua kuwa kipindi cha sensa hakipaswi kutumika kujitutumua na kuonesha madaraka bali ni namna ya kukusanya takwimu ili serikali ijipange kutoa huduma za msingi zinazotosheleza jamii.

Askofu huyo pia aliwakumbusha waumini kumpa Yesu nafasi katika maisha yao, mipango, uhusiano na matamanio yao ili wabadilishwe vipaumbele na mitazamo yao na kuwa watu wapya wakiwa pamoja na Kristo.

KABWELA Na Fadhili Mohammed



# Mabehewa mizigo 264 ya SGR yatua

**Na Elizabeth Zaya**

KATIKA kuboresha usafiri wa reli nchini, Shirika la Reli Tanzania (TRC) limesema limeshaleta mabehewa 264 yatakayotumika kubeba mizigo katika reli ya kisasa (SGR).

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano cha TRC, Fredy Mwanjala, mabehewa hayo yaliwasili juzi katika Bandari ya Dar es Salaam yakitokea China.

Mwanjala alieleza kuwa kazi ya ushushaji mabehewa hayo kutoka kwenye meli itakapokamilika, itafuata kazi ya kuyafanyia majaribio kwenye reli yakiwa tupu kisha yakiwa yamebeba mizigo.

"Mabehewa hayo yatakuwa yanatembea kwa kasi ya kilomita 120 kwa saa, majaribio hayo yatakamilika mara tu wataalamu wa TRC wakishirikiana na wale wa mkandarasi watakaporidhika kuwa utendaji kazi wa mabehewa hayo umekidhi viwango kulingana na mkataba. Tarehe rasmi ya kuanza operesheni za mabehewa hayo, shirika litaujulisha umma," alisema Mwanjala.

Kwa mujibu wa Mwanjala, kati ya mabehewa hayo 264 yaliyowasili, 200 ni ya kubeba makasha na 64 ni ya kubeba mizigo isiyofungwa.

Mwanjala alisema: "Shehena hiyo ya mabehewa 264 ni sehemu ya jumla ya mabehewa 1,430 ambayo kwa mujibu wa mkataba, yanatengenezwa na kampuni ya CRRC ya China."

Novemba 15 mwaka huu, TRC iliarifu umma kuwa utengenezaji mabehewa hayo 264 ya mizigo yatakayotumika katika reli ya SGR ulikuwa umekamilika nchini China, huku meli iliyobeba mabehewa hayo tayari ilikuwa imeng`oa nanga katika Bandari ya Dalian, China Novemba 12 mwaka huu. Kwa mujibu wa TRC, katika kipindi hiki ambacho mabehewa hayo hayakuwapo, mizigo yenye uzito uliopitiliza haikuruhusiwa katika treni hiyo ya SGR ambapo abiria wa daraja la biashara alipaswa kuwa na mzigo usiozidi kilo 30, huku daraja la uchumi abiria alipaswa kuwa na mzigo usiozidi kilo 20.

TRC ilianza kutoa huduma za SGR kati ya Dar es Salaam na Morogoro Juni 14 mwaka huu na Julai 25 ilianza safari ya Dodoma.

Hivi karibuni Waziri wa Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa alisema kuwa tangu kuanza kwa huduma hiyo ya treni ya kisasa, mapato yaliyopatikana ni Sh. bilioni 15.69.

Prof. Mbarawa alisema kwa kipindi hicho, SGR imesafirisha abiria 645,421 katika safari zake za kutoka Dar es Salaam kwenda Morogoro na Dar es Salaam kwenda Dodoma.

Wiki iliyopita Msemaji Mkuu wa Serikali na Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Gerson Msigwa, alisema kuwa hadi kufikia Desemba 11 mwaka huu, abiria waliokuwa wamesafirishwa kwa treni za SGR walikuwa wamefikia 1,174,404.

*Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz*



Fundi umeme kitengo cha dharura kutoka Shirika la umeme Tanzania (TANESCO) Mkoa wa Shinyanga akifanya matengenezo ya umeme katika Mtaa wa Ndembezi Ubalaji Manispaa ya Shinyanga jana. **PICHA: MARCO MADUHU**

# 2,800 mbaroni Songwe, wengi watuhumiwa ukatili wa kijinsia

**Na Mwandishi Wetu**

JESHI la Polisi mkoani Songwe limesema kuwa katika kipindi cha Januari hadi Desemba mwaka huu limewakamata watuhumiwa 2,827 wa makosa mbalimbali kulinganisha na watuhumiwa 3,238 katika kipindi kama hicho mwaka jana.

Limesema wengi wa watuhumiwa hao ni wa matukio ya ukatili wa kijinsia, uvunjaji, wizi, mauaji, utapeli kwa njia ya mtandao, dawa za kulevya na ukiukwaji wa sheria za usalama barabarani.

Taarifa iliyotolewa na Jeshi la Polisi Songwe ilieleza kuwa kwa mwaka huu jeshi hilo limepata mafanikio makubwa kwa watuhumiwa wa makosa mbalimbali kuhukumiwa, 327 wakikutwa na hatia.

Imeelezwa katika taarifa ya jeshi hilo kuwa kati ya idadi hiyo, watuhumiwa 37 wamehukumiwa kifungo cha miaka 30 getrezani kila mmoja kwa kwa kosa la kubaka, 14 wamehukumiwa kifungo cha maisha gerezani kwa kosa la kulawiti na kubaka.

Vilevile, watuhumiwa 17 wamehukumiwa kifungo cha miaka 30 jela kwa kosa la unyang'anyi kwa kutumia silaha na watuhumiwa 12 wamehukumiwa kwenda jela miaka 20 kwa kosa la kukutwa na silaha ikiwa na risasi pamoja na nyara za serikali.

Imeelezwa katika taarifa hiyo kuwa watuhumiwa 227 wamehukumiwa kifungo cha mwaka mmoja mpaka miaka 15 kwenda jela kwa makosa mbalimbali yakiwamo ya ukiukwaji sheria za usalama barabarani.

Katika operesheni ya kukamata dawa za kulevya na pombe haramu, jeshi hilo limekamata watuhumiwa 129 wakiwa na lita 483 za pombe hiyo, watuhumiwa 43 walifikishwa mahakamani kwa makosa ya kukutwa na dawa za kulevya.

"Watuhumiwa hao walikutwa na bangi kilo 252 na gramu 475 katika wilaya za Momba, Ileje, Songwe na Mbozi na watuhumiwa 180 walihukumiwa kwenda jela miaka mitatu hadi mitano na kesi 72 zinaendelea kusikilizwa mahakamani," inaelezwa katika taarifa hiyo ya polisi.

*Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz*

# Daftari la Wapigakura kuboreshwa kuanzia kesho

**Na Mwandishi Wetu**

UBORESHAJI Daftari la Kudumu la Wapiga Kura katika mikoa ya Mbeya, Iringa na Dodoma katika Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa unatarajiwa kuanza kesho na kumalizika Januari 2 mwakani.

Hiyo ni kwa mujibu wa taarifa iliyowekwa katika tovuti ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC). Mwenyekiti wa tume hiyo, Jaji Jacobs Mwambegele amewataka washiriki wa mafunzo kwa waandishi wasaidizi na waendesha kifaa cha bayometriki wilayani Chunya, mkoa wa Mbeya kutekeleza majukumu yao kwa uaminifu ili kufanikisha uboreshaji wa daftari.

Alitoa agizo hilo juzi alipotembelea mafunzo kwa waandishi wasaidizi na waendesha kifaa cha bayometriki yaliyofanyika wilayani humo ikiwa ni maandalizi ya uboreshaji wa daftari la kudumu la wapiga kura.

Alisema kazi ya uboreshaji daftari ni muhimu kwa taifa kuelekea kwenye Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025, hivyo aliwataka washiriki hao wazingatie uaminifu katika kutekeleza majukumu yao.

"Kazi ya uboreshaji daftari ambayo mmepangwa kuifanya ni kazi muhimu kwa taifa letu tukielekea kwenye Uchaguzi Mkuu mwakani. Mimi niwasihi ndugu washiriki kwamba mmeamini kwenda kuitekeleza.

"Kwahiyo katika kutekeleza kazi hii mnahitajika kuwa waaminifu. Lakini pia lengo la kuwaleta hapa ni kuwafundisha na wengine tunawakumbusha ili kazi hii ikatekelezeke vizuri," alisema.

Aliwataka washiriki ambao ni wazoefu katika kutekeleza kazi hiyo wawafundishe vizuri ambao siyo wazoefu ili watakapokwenda kutekeleza jukumu hilo, kazi ifanyike vizuri.

Alisema endapo watakutana na changamoto zozote katika utendaji kazi wao, wasisite kuwasiliana na tume kwa ufafanuzi au kwa maelekezo mengine yoyote.

Mjumbe wa INEC, Dk. Zakhia Mohamed Abubakar aliwataka washiriki wa mafunzo hayo kuhakikisha wanaelewa wanayofundishwa ili waweze kutekeleza jukumu lao kwa weledi na ufanisi.

Alisema waandishi wasaidizi na waendesha kifaa cha bayometriki ni watendaji muhimu katika kufanikisha uboreshaji wa daftari kwa sababu wao ndiyo wataowaandikisha wapigakura.

Mwenyekiti wa mafunzo hayo, Isakwisa Kaminyoge ambaye ni mshiriki kutoka kata ya Mtanila, akiwa ni mwandishi Msaidizi, alishukuru waendeshaji mafunzo kwa kutoa mafunzo kwa weledi na kuwawezesha washiriki.



# Wanaharakati watoa angalizo matukio ukatili K'njaro

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

WANAHARAKATI wametoa tahadhari kwa wakazi wa miji ya Moshi, Hai, Siha na Rombo kuhusu matukio ya ukatili wa kingono, ubakaji na ulawiti wakati huu wa sikukuu za mwisho wa mwaka.

Wamesema miji hiyo kwa sasa imefurika maelfu ya watu wanaokwenda kwenye makazi yao ya asili kusherehekea sikukuu za mwisho wa mwaka.

Tahadhari hiyo ilitolewa juzi na mwanaharakati anayepambana na ukatili wa kijinsia mkoani humo, Veronica Ollomi, akiwataka wazazi/walezi, kujitahidi kutupia macho suala zima la ulinzi wa watoto katika sikukuu hizo.

Alikuwa akizungumza juzi na viongozi wapya wa serikali za mitaa na vijiji wa Wilaya ya Moshi, waliokuwa wakinolewa kupitia mradi wa Sauti ya Haki, unaotekelezwa na Shirika la KWIECO, kwa ufadhili wa Women Fund Tanzania Trust (WFT).

Mafunzo hayo yanahusu masuala ya jinsia na namna wanavyoweza kutumia nafasi zao kusimamia haki na usawa wa kijinsia katika maneo yao.

"Sisi kama wadau wa kupinga ukatili wa kijinsia, tunapenda kutoa wito kwa jamii kusherehekea sikukuu hizi kwa amani na utulivu lakini pia kujitahidi katika suala zima la ulinzi wa watoto.

**"Sisi kama wadau wa kupinga ukatili wa kijinsia, tunapenda kutoa wito kwa jamii kusherehekea sikukuu hizi kwa amani na utulivu lakini pia kujitahidi katika suala zima la ulinzi wa watoto**

"Kwa sababu watoto ndiyo mara nyingi waathirika wakubwa wa masuala ya ukatili wa kijinsia, ikiwamo ubakaji, ulawiti. Inawezekana matumizi ya vilevi kupita kiasi vinaweza kusababisha mtu akapata ushawishi wa kumbaka mtoto au kumlawiti mtoto.

Kwa hiyo tunaomba jamii isherehekee sawa sikukuu vizuri lakini pia wahakikishe kama wazazi, kwa sababu kuna kawaida watoto kuruhusiwa kutoka kwenda kutembea, hebu wazazi wahakikishe ulinzi wa watoto wao ili waendelee kuwa salama na kuhakikisha kwamba unajua mwanao anakwenda wapi.

Zaidi alifanufua: "Kama unamwachia kwenda kutembea hakikisha unajua mahali anapokwenda kutembea, kwa sababu dunia ya sasa hivi siyo salama, watoto wengi hawako salama. Kwa hiyo tunaomba sana wazazi wazingatie hilo ili tumalize mwaka vizuri na mwakani watoto waweze kuendelea na masomo yao kama kawaida."

Kwa mujibu wa Veronica, maeneo mengi ya starehe, wazazi na walezi wengine wanakwenda na watoto, kitu ambacho kisheria hakiruhusiwi.

Mwanaharakati kutoka Kata ya Mwika Kusini, Easther Temba alieleza namna wakazi wa kata hiyo, wanavyostaajabishwa na kuchukizwa na kitendo cha wazazi, kumwachia mtoto anayesoma darasa la awali (jina limehifadhiwa) kuzurura katika maeneo ya starehe na kurudi nyumbani kati ya saa 5 mpaka saa 6 usiku.

Temba alisema: "Tunajiuliza ni wapi yupo, kumbe yuko kwenye vilabu vya pombe wanakocheza korokoro na kamari (michezo ya kuhabatisha).

Sasa huko huko kumbe vijana wanamchukua huyo mtoto na kumrubuni na kumfanyia vitendo vya kikatili ambavyo sivyo. Na yule mtoto anaenda kuwaambia wenzake twendeni niwafundishe ninavyofanyaga." Alisema

Kata zilizonifaika na mafunzo hayo ni Mwika Kusini, Mwika Kaskazini, Kiruavunjo Kusini, Mabogini, Pasua na Mfumuni.



Muuza kuku akipatana na mteja wake katika soko wilayani Muheza mkoani Tanga jana, katika Sikukuu ya Krismasi. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Serikali yabeba mzigo ununuzi mitungi ya gesi

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

SERIKALI imekubali kubeba asilimia 50 ya gharama za ununuzi wa mitungi ya gesi ya nishati safi ya kupikia, ambayo imekuwa mzigo kwa wananchi wa kawaida, wanaotamani kuondokana na matumizi ya kuni na mkaa.

Hivyo, mwananchi badala ya kulipia mtungi mmoja kwa Sh. 35,000 katika Mkoa wa Tanga hivi sasa atawajibika kulipa 17,500.

Neema hiyo ilitangazwa juzi mkoani Tanga na Mkurugenzi wa Teknolojia za Nishati Jadilifu na Mbadala Vijijini, kupitia Wakala wa Umeme Vijijini (REA), Advera Mwijage.

Kwa mujibu wa Mwijage, mradi huo unatekelezwa katika Wilaya nane za Mkoa wa Tanga.

"Kwa mfano katika Mkoa wa Tanga, mtungi mmoja ni shilingi 35,000 lakini kwa kutambua kwamba wananchi wengi wanatamani kutumia nishati hii na hawana uwezo wa kumudu gharama. "Serikali italipia asilimia 50, ambayo ni shilingi 17,500 na mwananchi atalipia shilingi 17,500. Nia ni kuhakikisha wananchi wanaondokana na uharibifu wa mazingira na kulinda afya zao, kwa kuepuka uzalishaji wa hewa ya ukaa."

Mwijage, alisema kampuni iliyopata fursa ya kusambaza mitungi hiyo ni Manjis, ambayo katika wilaya nane, kila moja itapata mitungi 3,255. Mkoa wa Tanga, utapata jumla ya mitungi 26,040 kwa garama ya shilingi milioni 455.7.

Alisema: "Kikubwa zaidi anachotakiwa awe nacho ni kitambulisho cha taifa, kwa sababu sisi kama serikali, baadaye tutafuatilia kujua ni akina nani wanatumia nishati hii na hili ndio lengo ili ifikapo mwaka 2034 Watanzania asilimia 80 waweze kutumia nishati safi".

# Bilioni 16/- kupunguza vifo vya watoto ifikapo 2030

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MRADI wa Newborn Essential Solutions and Technology (NEST 360), umetoa Dola za Marekani milioni 7.1 (Sh.bilioni 16.9) kwa serikali ya Tanzania kwa ajili ya kupunguza vifo vya watoto wachanga ifikapo mwaka 2030.

Tanzania ni moja ya nchi iliyojidhatiti kufikia malengo endelevu ya kimataifa (SDG 3.2), kupunguza vifo vya watoto wachanga, chini ya 12 kwa kila vizazi hai 1,000 ifikapo mwaka 2030.

Akiwa katika Mji wa Moshi, mkoani Kilimanjaro, Mkurugenzi wa Taasisi ya Afya Ifakara, ambaye pia ni kiongozi wa mpango wa NEST 360, Dk. Honorati Masanja, ameeleza kuwa fedha hizo zitatumika kutekeleza awamu ya pili ya mpango huo wa sekta ya afya.

"Awamu ya kwanza ni ile iliyoanza mwaka 2019 hadi 2023. mpango wa NEST 360 kwa kushirikiana na Wizara za Afya, ulitekeleza kifurushi kamili cha afua kwa huduma za watoto wachanga.

"Ambapo matokeo yanaonyesha matumaini, kwa kuwa zaidi ya watoto 100,000 kwa mwaka katika hospitali 68 zilizoko nchi za Malawi, Tanzania, Kenya, na Nigeria wamenufaika na mpango huu,"alisema.

Kwa mujibu wa Masanja, ufadhili huo utazinufaisha hospitali 28, ambapo 25 kati ya hizo, ziko katika mikoa minne ya Tanzania Bara, na Hospitali tatu ziko Visiwani Zanzibar.

Mpango wa NEST, unahusisha ukarabati miundombinu, ununuzi wa vifaa vya tiba, kujenga uwezo kwa madaktari na wahandisi wa vifaa tiba, ili kutoa huduma bora, ufuatiliaji wa ubora wa huduma za watoto wachanga.

Akizungumzia uwezeshaji huo, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, alisema vifo vya watoto wachanga bado ni changamoto.

"Serikali ya Tanzania katika kushughulikia changamoto hii, mwaka jana serikali ilitumia Dola za Marekani milioni 18, kwa ukarabati wa vyumba vya watoto wachanga na ununuzi wa vifaa muhimu vya matibabu.

Hata hivyo, bado kuna kazi kubwa mbele yetu, tunajitaji huduma zaidi kufikia vituo vingi zaidi na kuokoa maisha ya watoto wachanga wengi zaidi."





# Wachangishana kukarabati miundombinu

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAKAZI wa Mtaa wa Sofi Kata ya Mhongolo Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga wamelazimika kuchanga fedha kila kaya kukarabati barabara inayounganisha mtaa wao na Kata ya Busoka baada ya kuharibiwa na mafuriko.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, baadhi ya wakazi hao, akiwemo Neema Toi , alisema ubovu wa miundombinu hiyo umekuwa ukisababisha wanakosa huduma za dharura hasa kwa wagonjwa na wajawazito wakati wa mvua.

Neema, alisema wamekuwa wakipata kero wakati wa mvua za masika kutokana na barabara hiyo kujaa maji na wanafunzi kukosa masomo kwa kushindwa kwenda shule.

Alisema wajawazito nao wamekuwa wakishindwa kuhudhuria kliniki na wengine kulazimika kujifungulia majumbani, hivyo kuhatarisha maisha yao.

Mkazi mwingine Mathias Mwita, alisema gharama za usafiri zimeongezeka kutoka Sh.1,000 mpaka Sh.2,000 kwa pikipiki na maji kutokana na ubovu wa barabara hiyo.

Mwita, alisema kuna vijana wanajiajiri kwa kuvusha watu kwa kuwabeba mgongoni na kulipwa ujira.

Alisema kipindi cha mvua za masika baadhi yao wamekuwa na tabia ya kutiririsha maji taka kwenye barabara hiyo na kutishia kutokea kwa mlipuko wa magonjwa hasa kwa watoto.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Mhongolo, Emmanuel Nangale alisema wanaendelea kuhamasisha wananchi kuchanga fedha kwa ajili ya ukarabati huo.

Meneja wa Wakala wa Barabara Mjini na Vijijini (TARURA) Wilaya ya Kahama, Joseph Mkwizu, alisema mwaka 2023/24 walitenga Sh.milioni 63 kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Busoka inayounganisha mawasiliano na barabara hiyo.

Kwa mujibu wa Mkwizu, walijenga makalavati mawili, kuchonga barabara na kuweka changarawe.

Alisema Barabara ya Sofi imekuwa korofi kila mwaka kwa sababu ya kupokea maji ya mvua mara kwa mara.

Mkwizu, alisema wameomba fedha katika bajeti ya mwaka ujao wa fedha wa 2025/26 kwa ajili ya kukarabati sehemu korofi.

Alisema barabara hiyo inayounganisha Mtaa wa Sofi, Mhongolo na Kata ya Busoka inapitisha asilimia 85 ya wanafunzi wa Shule ya Msingi Bomani, Sekondari ya Nyashimbi na ni tegemeo kwa wakazi hao kwenda kwenye shughuli zao za kiuchumi.

# Wazawa waitwa kusuluhisha koo

**Na Ambrose Wantaigwa,** TARIME

WAZAWA wa wilayani hapa Mkoa wa Mara wanaofanyakazi maeneo mengine nchini wametakiwa kutumia nafasi zao kutokomeza uhasama baina ya koo 12 na kushiriki katika shughuli za kiuchumi.

Wito huo ulitolewa juzi na wazee pamoja na viongozi wa kutoka wilayani hapa wakati wa harambee ya kuchangia kikundi cha kuweka na kukopa fedha cha jamii ya Wakurya (KSG) kinacholenga kuimarisha uchumi wa jamii hiyo.

Akizungumza wakati wa harambee hiyo, aliyewahi kuwa Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mara Samwel Kiboye maarufu kwa jina la'namba tatu', aliwataka idadi kubwa ya wananchi wenye asili yao wanaofanya kazi serikalini na sekta binafsi watumie nafasi zao kulinda maridhiano baina ya koo hizo ili wakazi wa maeneo hayo washiriki katika maendeleo na kuacha migogoro. Aliwataja baadhi ya wazawa mashuhuri wanaoweza kuwa mabalozi wa amani kwa kutumia nafasi zao serikalini kuwa ni pamoja na mbunge wa zamani wa Tarime na mchapishaji vitabu maarufu, Nyambari Nyangwine.

**Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria, Eliakim Maswi, Waziri wa zamani wa Kazi, Ajira na Vijana, Gaudensia Kabaka, Mkuu wa Wilaya ya Tunduru...**

Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria, Eliakim Maswi, Waziri wa zamani wa Kazi, Ajira na Vijana, Gaudensia Kabaka, Mkuu wa Wilaya ya Tunduru, Simon Chacha na Mkuu wa Majeshi Mstaafu, Jenerali George Waitara.

Alisema taswira ya usalama ya Wilaya ya Tarime siku za nyuma ilikabiliwa na changamoto za vita ya koo na wizi wa mifugo hali iliyopelekea kuanzishwa kanda maalum ya kipolisi Tarime na Rorya.

Alisema kwa sasa hali imebadilika usalama umeimarishwa, wananchi wanashirikiana na viongozi wa serikali na sekta binafsi kufanya kazi kwa bidii ili wajipatie kipato na maendeleo.

"Tunahitaji mabalozi wa kulinda na kuhamasisha amani iendelee kuwepo," alisema Kiboye.

Alisema kwa kutumia ushawishi wa viongozi na wafanyabaishara, wilaya hiyo itapiga hatua kuelekea maisha bora bila uvunjifu wa amani kama miaka ya nyuma.

Mwenyekiti wa kikundi hicho, Lucas Magoti, alisema zaidi ya Shilingi milioni 13 zilipatikana katika harambee hiyo.

Magoti, alisema wanalenga kuwaleta karibu watu wote wanaotoka Tarime na Mara kuhakikisha wanafanya shughuli za kuliingizia taifa na wao kipato na kuachana na migogoro ya kikoo na kikabila.



Paroko Msaidizi wa Kanisa Katoliki Parokia ya Mtakatifu Karoli Luhanga, Nyegezi Jimbo Kuu la Mwanza, Padre Switbert Massao akibariki mfano wa eneo la zizi alipozaliwa Yesu Kristo wakati wa misa ya mkesha wa Krismasi juzi. **PICHA: VITUS AUDAX**

# Uwanja wa ndege kukamilika mwakani

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MRADI wa upanuzi wa uwanja wa Ndege Ibadakuli katika Manispaa ya Shinyanga, mkoani hapa unatarajiwa kukamilika Aprili mwakani na kuanza kutoa huduma kwa wananchi.

Hayo yalibainishwa juzi na Mhandisi Ruburi Kahatano wa Kampuni ya Chico, inayotekeleza mradi wa ujenzi huo, wakati wa ziara ya waandishi wa habari mkoani hapa.

Kahatano, alisema ujenzi wa uwanja huo umefikia asilimia 80 na kwamba utakamilika kulingana na mkataba. Alisema hadi sasa kuna ndege mbili za dharura zimetua, moja kwa ajili ya kubeba mgonjwa kumpeleka Hospitali ya Mloganzila jijini Dar es Salaam.

Alisema mgonjwa huyo alitakiwa kwenda kupata matibabu zaidi ya kibingwa na kuokoa maisha yake.

Kahatano, alisema ndege nyingine ilitua uwanjani hapo kwa ajili ya kumleta mfanyakazi wa kampuni moja mkoani hapa.

"Uwanja huu kwa ndege mchana zinaweza kutua, lakini usiku haziwezi sababu bado hatujafunga taa,"alisema.

Mhandisi Chiyando Matoke wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) Mkoa wa Shinyanga, wasimamizi wa ujenzi wa uwanja huo, alisema hadi kukamilika, utagharimu Sh.bilioni 44.8.

Mwenyekiti wa Klabu ya Waandishi wa Habari Mkoa wa Shinyanga, Greyson Kakuru, alisema katika ziara hiyo wameshuhudia kazi kubwa ambayo inafanywa na serikali ya ujenzi wa miradi ya kimkakati.

Kakuru, alisema kukamilika kwa upanuzi wa uwanja huo, kutafungua fursa za kiuchumi katika mkoa huo wa Shinyanga.

ama
ALHAMISI DESEMBA 26, 2024
AFYA NA MAZINGIRA







AFYA

# Vita vya 'unga' Umoja Mataifa, AU hadi Samia afikia mfano wa kuigwa

**Na Tuntule Swebe**

NAMNA ya kuendesha maisha katika uhalisi wa kawaida, ina hatua inayopanda hadi mamlaka ya nchi, serikali na mkuu wake, vyote vikimrahisishia maisha mkazi, pia viumbe vingine kadri inavyowezekana.

Upande wa pili, kuna tafsiri inayomgusa moja kwa moja raia wa kawaida katika mwenendo wake wa kila siku. Hapo kuna dhana inayoitwa 'watu kwenda na wakati' wakijifunza matumizi ya vitu mbalimbali kama kompyuta zinazowarahisishia kazi.

Vilevile katika mageuzi hayo, kuna watu wanaofanya visivyostahili, wakiamini 'ni mitindo ya kisasa.' Hapo nako ndiko kuna hadithi kama matumizi ya pombe kupindukia, hali kadhalika dawa za kulevya, hatari kubwa kiafya.

Majumuisho ya misukumo ya fikra hizo, mtu anapotumia dawa za kulevya kwa falsafa ya 'kwenda na wakati', vyanzo vikuu vinavyomshawishi vikiwa vyombo vya mawasiliano; simu, televisheni, radio, simu na kompyuta inaibua mfumo mpya wa maisha.



Aliyekuwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Justine Masejo, akiwa na dawa za kulevya zilizoshikwa mkoani humo, Machi mwaka 2022. **PICHA: MTANDAO**

**DAWA ZA KULEVYA ZIKOJE?**

Dawa za kulevya ni kemikali, ziingiapo mwilini, huathiri ubongo wa mtumiaji na kumsababishia kuwa na matendo, hisia, fikra na mwonekano tofauti na matarajio ya jamii.

Kemikali hizo hutokana na mimea na madini ambayo ni malighafi muhimu kwa mahitaji mengine ya mwanadamu. Hizo zinapoingia mwilini kwa njia kuu tatu: Kunywa; kuzila dawa zisizoruhusiwa kama bhangi na mirungi, cocaine, heroin na mandrax; pia zinazoruhusiwa kwa tiba hospitali.

Umoja wa Mataifa unataja, zaidi ya watu milioni 296 walitumia dawa za kulevya mwaka 2021, ikiwa ni ongezeko la asilimia 23 kulinganisha na miaka 10 iliyotangulia, zikinukuu Ripoti ya Ofisi ya Umoja wa Mataifa inayohusika na Kupambana na Dawa za Kulevya na Uhalifu - UNODC.

Takwimu mpya zikaweka makadirio ya kimataifa ya watu wanaojidunga dawa za kulevya kwa mwaka 2021 kwamba ni milioni 13.2; asilimia 18 juu kuliko ilivyokadiriwa awali.

Ripoti hiyo inaeleza zaidi kwamba, idadi ya wanaougua shida za matumizi ya dawa za kulevya imepanda, kufika watu milioni 39.5, sawa na ongezeko la asilimia 45 katika kipindi cha miaka 10.

UNODC inaangaza jinsi ukosefu wa usawa wa kijamii na kiuchumi, unavyosukumwa na changamoto za dawa za kulevya; uharibifu wa mazingira na ukiukwaji wa haki za binadamu, ukichangia pia, kuongezeka dawa za kulevya zinazotengenezwa viwandani.

**SURA YA TIBA**

Mahitaji ya kutibu magonjwa yanayohusiana na dawa za kulevya yanaelezwa na Umoja Mataifa hayajafikiwa, wastani ukiwa mtu mmoja kati ya watano, wanaougua matatizo hayo (mwaka 2021) huku tofauti zinaongezeka katika upatikanaji tiba maeneo yote duniani.

Hapo kundi la vijana linatajwa kuwa hatarini zaidi kutumia dawa za kulevya, pia huathiriwa na magonjwa yanayohusu matumizi ya dawa hizo duniani. Barani Afrika kunatajwa kwamba, asilimia 70 ya wanaopata matibabu ya dawa za kulevya, wako chini ya umri wa miaka 35 au kwa lugha rahisi ni vijana.

Ripoti inashauri afya ya umma, kinga na ufikiaji huduma za tiba, zipewe kipaumbele duniani, vinginevyo changamoto za dawa za kulevya zitaumiza wengi.

Kuna msisitizo unaotaja hatua za utekelezaji sheria, kuendana na mbinu za kudhibiti biashara ya uhalifu wa kisasa wa dawa za kulevya za bei nafuu zinazotengenezwa viwandani, ambazo ni rahisi kuletwa sokoni.

Mkurugenzi Mtendaji wa UNODC, Ghada Waly anafafanua: "Tunashuhudia kuendelea kuongezeka kwa idadi ya watu wanaokabiliwa na matatizo ya matumizi ya dawa za kulevya duniani kote, huku matibabu yakishindwa kuwafikia wote wanaohitaji.

"Tunahitaji kuongeza hatua dhidi ya makundi ya biashara ya dawa za kulevya yanayotumia mizozo na migogoro ya kimataifa, kupanua kilimo na uzalishaji haramu wa dawa za kulevya, hasa ya dawa za viwandani, kuchochea masoko haramu."

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Guterres, anatumia fursa hiyo kuisihi jamii kutowatenga waathirika wa dawa za kulevya, akiitaka jumuiya ya kimataifa kuendelea kukomesha matumizi mabaya na ulanguzi wa dawa za kulevya.

**SAMIA ANASIFIWA**

Ndani ya hoja hiyo na harakati zake, kwa mustakabali wa Tanzania, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, anazitaka wizara zinazohusika na maendeleo ya jamii, pia asasi za kiraia.

Vilevile kuna suala la wazazi na walezi kuwekeza nguvu, kulinda jamii zao na kuendelea kudhibiti uingizaji, uzalishaji, usafirishaji na utumiaji dawa za kulevya.

Ni tamko lake Rais Dk. Samia katika Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha, Juni mwaka jana, katika kilele cha Maadhimisho Siku ya Kupiga Vita Dawa za Kulevya Duniani iliyobeba kaulimbiu 'Zingatia Utu, Imarisha Huduma za Kinga na Tiba."

Akasisitiza: "Kinga ni bora kuliko tiba, hivyo natoa wito kwa mamlaka husika, taasisi za serikali na asasi za kiraia kuongeza jitihada kwenye kutoa elimu kwa jamii hasa vijana wajiepushe na matumizi ya

Inaendelea Uk. 12

AFYA

# Bingwa Dk. Mngumi na darasa la unywaji sahihi maji yasikudhuru

## •Chanzo magonjwa kibao; hesabu ya kujisaidia kwa siku
## •Inapokosewa kanuni, yakaribisha majanga yafuatayo...

**Na Christina Mwakangale**

JUZI Jumanne, gazeti hili lilikuwa na ufafanuzi namna ilivyo thamani ya maji, ikiendana na tahadhari ya ama kuzidisha kunywa au kupunguza mahitaji, huangukia madhara. Fuatilia...

DK. JONATHAN Mngumi, Tabibu Bingwa wa Magonjwa ya Ndani na mbobezi wa magonjwa ya figo, katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), ana darasa zaidi kuhusu kiwango cha unywaji maji kuzingatia mazingira, aina ya kazi.

Huku akiendeleza anagalizo lake la juzi 'kutopitiliza unywaji maji,' anadadavua jinsi maji yanavyopunguza ukavu wa ngozi, kudumisha afya ya viungo kama magoti na viwiko, akihimzia 'tii kiu yako kwanza, kabla ya kunywa maji.'

Bingwa huyo anayeongoza Kitengo cha Magonjwa ya Figo, katika maelezo yake kwa Nipashe wiki hii, anataja mbinu, faida na athari za kutokunywa maji pamoja na mfumo mzima wa figo na mkojo.

"Faida za maji ya kunywa kwa binadamu, kwanza maji ni muhimu kwa uhai na afya ya mwili. Faida zake ni uwezo wa kutoa sumu mwilini, maji husaidia figo kuchuja taka na sumu kutoka kwenye damu na kuzitoa kupitia mkojo," anasema bingwa huyo

Dk. Mngumi, anafafanua kuwa maji yanasaidia mzunguko wa damu, kudumisha ujazo wake na kupunguza hatari ya magonjwa ya moyo na shinikizo la damu.

Pia, maji yanasaidia kuboresha na kufanikisha mmeng'enyo wa chakula, ikizuia tatizo la kufunga choo na inadhibiti joto la mwili.

"Maji husaidia kupooza mwili kupitia jasho, hasa wakati wa joto kali au mazoezi, kulainisha viungo na kuimarisha ngozi. Hupunguza ukavu wa ngozi na kudumisha afya ya viungo kama magoti na viwiko," anasema.

### KIASI KINACHOHITAJIKA

Bingwa huyo anasema, mtu mzima anayefanya kazi nzito juani au kutokwa jasho jingi, anashauriwa kunywa maji kati ya lita tatu hadi tano kwa siku, kulingana na kiwango cha jasho na unyevunyevu wa mazingira.

Anasema, mbinu ya upimaji maji na namna ya kunywa ni angalau glasi moja hadi mbili za maji kila saa. Vilevile, kila baada ya saa moja ya kufanya kazi nzito, anatakiwa kunywa takribani millilita 500 (nusu lita) mpaka lita moja za maji.

Dk. Mngumi anabainisha, iwapo kiu ni zaidi au mkojo una rangi tofauti, akitoa mbinu ya kuchunguza kuwa: "Ikiwa mtu anajisikia kiu sana au mkojo wake ni wa rangi ya njano iliyokolea, ni dalili ya ukosefu wa maji mwilini na anapaswa kuongeza unywaji wa maji."

### UNYWAJI USIO SAHIHI

Dk. Mngumi anaeleza athari za unywaji duni wa maji, akisema unaweza kuathiri viungo kadhaa ambavyo ni muhimu.

"Figo; ukosefu wa maji huongeza hatari ya mawe kwenye figo (kidney stones), maambukizi ya njia ya mkojo (UTI) na kushindwa kufanya kazi ipasavyo.

"Ngozi; ukosefu wa maji hufanya ngozi kuwa kavu na kuharakisha kuzeeka,"anatamka na kuendelea:"Moyo; huongeza mzigo kwa moyo kwa sababu ya kupungua kwa ujazo wa damu, jambo linaloweza kusababisha shinikizo la damu."




Dk. Jonathan Mngumi, Tabibu Bingwa wa Magonjwa ya Ndani, na Figo, na anayeongoza kitengo cha magonjwa hayo, katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

Mtaalamu huyo anaendelea: "Ubongo; upungufu wa maji unaweza kusababisha maumivu ya kichwa, kutoelewa vizuri na uchovu.

"Mmeng'enyo wa chakula; Unywaji duni husababisha kufunga choo na kuongeza asidi (tindikali) tumboni, jambo linaloweza kusababisha vidonda vya tumbo."

### WASTANI WA KUJISAIDIA

Dk. Mngumi anataja idadi ya safari za kwenda haja ndogo kwa saa 12 hadi 24, kwa mtu kila siku akiainisha kwa lugha: "Kwa mtu mwenye afya njema, kujisaidia haja ndogo mara nne hadi saba kwa siku ni kawaida. Sawa na kila baada ya saa tatu hadi nne.

"Kwa saa 12 kujisaidia mara mbili hadi nne, kwa saa 24, kujisaidia mara nne hadi saba7, kulingana na kiwango cha unywaji maji na shughuli za mwili ni kawaida.

"Ishara za tatizo ni ikiwa mkojo ni wa rangi ya njano iliyokolea au kujisaidia ni mara chache sana (chini ya mara nne kwa siku), huenda mtu anakunywa maji 'machache' (kidogo)."

### UNYWAJI DUNI

Bingwa huyo anasema kuna athari ya kutokunywa maji, akiutolea maelezo kuwa "unywaji duni wa maji, huathiri mfumo wa mkojo kuanzia kwenye figo hadi kibofu, pamoja na figo.",

Anataja eneo lingine la tatizo ni kwenye hatari ya kutengeneza mawe kwenye figo na husababisha kushindwa kuchuja sumu ipasavyo, jambo linaloweza kusababisha matatizo ya figo sugu (CKD).

"Mirija ya mkojo (Ureter) huathiriwa, ukosefu wa maji huongeza uwezekano wa maambukizi ya njia ya mkojo (UTI), hasa kwa wanawake," anaeleza.

### KIWANGO MAJI, KIBOFU

Dk. Mngumi anasema, kutokunywa maji kwa usahihi, kunasababisha maambukizi kutokana na mkojo kukaa muda mrefu kibofuni bila kutolewa.

Pia, anataja kupunguza uwezo wa kibofu kufanya kazi inavyotakiwa, jambo linalosababisha hisia ya haja ndogo mara kwa mara.

"Kunywa maji ya kutosha kila siku ni muhimu kwa afya ya mfumo wa mkojo na mwili kwa

Inaendelea Uk. 13

## Vita vya 'unga' Umoja Mataifa, AU hadi Samia afikia mfano wa kuigwa

Inatoka Uk. 11

dawa za kulevya, lakini sisi serikali tumejipanga vyema kukabiliana na janga hili."

Rais Dk. Samia, pia akaipongeza Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA), kufanya kazi nzuri ya kudhibiti uingizaji dawa hizo kitaifa.

Katika tukio hilo, Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA), iliwaelimisha wananchi waliotembelea kuhusu shughuli wanazozifanya, wakiwapima wahitaji na kutambua aina ya dawa hizo kutoka kwa waathirika kama heroin, bhangi na mirungi. Pia, wakawatambua watumiaji wapya.

Wakati kuna ufafanuzi huo wa mwaka jana wa mkuu wa nchi, mwezi huu Tanzania chini ya uongozi wake tena umemwagiwa sifa ya mafanikio kimataifa kupambana kukabili dawa za kulevya.

Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Ummy Nderiananga, ametoa kauli hiyo jijini Arusha akifungua Mkutano wa Siku Nne wa jukwaa lililo chini ya Umoja wa Afrika (AU), Tanzania ikitajwa kuwekeza zaidi kwenye kinga.

Anafafanua, maeneo yanakojengwa vituo vya kutoa huduma za afya kwa waraibu wa dawa hizo ni katika hospitali za kanda na rufani, makundi yakielimishwa, ikiwamo vilabu vya vijana shuleni.

Jukwaa hilo lina mikakati kupunguza uhitaji na usambazaji dawa za kulevya kwa nchi wanachama wa AU, Naibu Waziri anautaja ni mkutano unaotoa fursa ya kubadilishana uzoefu wa masuala ya afya, katika vita hivyo kukabili shida ya dawa za kulevya.

Naibu Waziri anataja mafanikio yametokana na kazi inayofanywa na Rais Dk. Samia, kuwekeza kwenye Sekta ya Afya, hususan ujenzi wa Vituo vya Tiba Saidizi kwa waathirika wa dawa za kulevya (MAT CLINICS) vinavyosimamiwa na serikali.

"Tumepiga hatua zaidi katika udhibiti wa dawa hizi nchini na wenzetu Nchi za Umoja wa Afrika, kuungana kwa pamoja katika kudhibiti matumizi ya dawa za kulevya, kudhibiti mbinu wanazotumia wauzaji na watumiaji wa dawa hizo na uimarishwaji wa maeneo ya mipakani, kuzuia uingizwaji dawa hizo nchini kwetu,"anasema.

Anasema hatua zaidi zinaendelezwa na serikali kudhibiti matumizi ya dawa za kulevya mitaani, sambamba na hatua za kisheria zinazochukuliwa.

"Jitihada za kudhibiti dawa hizi haziwezi kufanikiwa bila kushirikiana na nchi wanachama wa Umoja wa Afrika ambazo ni nchi zote za Bara la Afrika zikiwamo Namibia, Botswana, Zambia, Nigeria, Kenya na Sierra Leone.

"Kwa Tanzania kwa sasa tumeanzisha kituo cha utoaji huduma (Call Centre), ambako mwananchi ana uwezo wa kupiga simu kutoa taarifa za uwapo wa dawa za kulevya au viashiria, ili uchunguzi ufanyike na wahusike wachukuliwe hatua," anasema Nderiananga

Katibu Mkuu Msaidizi, Mipango, Sera za Kimataifa anayeshughulikia Ofisi ya Afrika na Mashariki ya Kati katika Masuala ya Kimataifa ya Utekelezaji wa Sheria, (INL) Maggie Nadri anasema vifo vinavyotokana na matumizi ya dawa za kulevya yaliyopitiliza vimepungua kwa asilimia 12 katika nchi za AU.

"Ni wakati sasa wa kuongeza nguvu eneo la utoaji elimu kwa vijana shuleni, vyuoni ili kupunguza matumizi ya dawa hizi kwa kuwajengea uwezo wataalam wa afya na mamlaka za ulinzi kubadilishana mbinu za kudhibiti matumizi ya dawa hizo katika maeneo ya mipakani, majini, ardhini na kwingineko ili kuwezesha wananchi wengi kutojiingiza katika dawa za kulevya," anahitimisha Maggie.

AFYA

WATAALAMU NA KAMPENI MBADALA...

# Wanaume nao kufunga kizazi, ukiwa mbadala kuwaunga wenza kinamama

**Na Joyce Lameck**

MATUMIZI ya njia za uzazi wa mpango, unatajwa si jukumu la mwanamke pekee, bali jambo linalobeba usawa wa kijinsia.

Hapo wanaume nao wana njia za uzazi wa mpango wanazoweza kuzitumia, katika kuwapuguzia wanawake majukumu na adha ya kupata matatizo ya kiafya.

Wajibu wa wanaume ni kuwasaidia wanawake kutumia njia za uzazi wa mpango, ili kutokomeza kupata mimba zisizotarajiwa.

Ni hatua muhimu inayowasaidia wanawake kupata afya bora ya uzazi na kuleta manufaa kwa jamii kiujumla, katika sura pana kitaifa.


Mara zote imekuwa kawaida kwa wanaume, kuwaachia wanawake zao mambo yote yanayohusiana na uzazi.

Ni mtazamo unaotawala kwamba, si jambo la wanawake pekee, wala si wanaume, lakini uhalisia ni kwa wanaume wanapaswa kushiriki vema mambo ya uzazi wa mpango.

Wataalamu afya na mamlaka zenye dhamana kwa kuliona hilo, wameendelea kutoa elimu ya matumizi sahihi ya uzazi wa mpango.

Pia, nafasi ya wanaume katika kutumia uzazi wa mpango, kuwezesha uzazi salama kwa mama pamoja na mtoto.

Hata hivyo, mbali na elimu hiyo, pia kunatajwa hitaji kufunga uzazi, pindi wanapofikia ukomo wa kuhitaji watoto, ili kuepuka mimba zisizo tarajiwa kwa wakati usio sahihi.



Elimu ya uzazi wa mpango ikiendelea

**WATAALAMU HUDUMA**

Kwa mujibu wa mtaalamu kutoka Manispaa ya Mkoa wa Kahama, Dk. Noel Malaki, anasema idadi ya wanaume wanaohudumia katika masuala ya uzazi wa mpango ni ndogo, ikilinganishwa na idadi ya wanawake katika mji huo.

Akifafanua, anasema kutokana na uhaba wa elimu kuhusu kufunga uzazi kwa wanaume haijatolewa ipasavyo, hivyo ni sababu inayochangia kutotumiwa na wadau wa kutosha.

Vilevile, Dk Malaki anataja matumizi ya uzazi wa mpango kuwa duni nako kunachangia kutoaminika kwake, kuwa njia sahihi, baadhi wakihofia uwezekano wa walakini katika tendo la ndoa kama awali.

Anataja mtazamo kwamba, baadhi ya njia za uzazi wa mpango ambazo mwanaume anaamini ni pamoja na matumizi ya kondomu, pia kutoa mbegu za kiume nje wakati wa tendo hilo, mwanamke akiwa kwenye siku za hatari kushika mimba.

Vilevile Dk. Malaki anataja kuwapo hali ya kufanyika upasuaji mdogo kwa lengo la kufunga mrija inayosafirisha mbegu za kiume; kitaalamu inaitwa (vasectomia).

Ni utaratibu wa upasuaji wa kufunga kizazi kwa mwanaume, walau miezi mitatu. Pia, viwango vya kutofaulu katika hatua hiyo, vinatajwa ni takribani moja kati ya 2000.

Hiyo kwa ujumla, inaorodheshwa ni njia ya kudumu ya kupanga uzazi kwa sababu, inamfanya mtu asiweze kuzaa tena.

**UTATA UZAZI WA KIUME**

Dk Malaki, anasema ingawa kuna njia za kurejesha uzazi wa kiume, kuna mbinu ya kuchukua mapema mbegu ya kutunga baadaye mimba nje ya mwili (invitrofertization).

Hilo linashauriwa kwa vijana wasio na watoto, kwa sababu uwezekano wa kughairi, baadaye ni mkubwa zaidi.

Mtoa Huduma Ngazi ya Jamii, Clement Masonga, anasema huduma hiyo imekuwa ngumu kwa wanaume wengi, wanaokosa taarifa sahihi za ufungaji kizazi kwa wanaume, ndiyo sababu inayowafanya kushindwa kuitumia.

Anashauri nafasi ya wanaume kusaidia fedha za usafiri kwenda kulipia njia za uzazi wa mpango, ikiwamo mahudhurio ya kliniki, matumizi ya kondomu na nyenzo nyinginezo.

Mtaalamu huyo anasema, pamoja na wanaume wengi kuogopa kutumia njia hiyo, lakini uhalisia ndio njia rahisi na salama.

**MNUFAIKA WA HUDUMA**

Mnufaika wa huduma ya kufunga uzazi kwa wanaume na mkazi wa Kahama (jina tunalo), anaeleza alivyoitumia njia hiyo, baada ya kupatiwa elimu sahihi akinena akagundua haina madhara ya kushiriki tendo la ndoa na mkewe.

"Nilikubali kufunga kizazi kutokana na faida ambazo hapo awali sikuzifahamu. Pia, nilihofia kuwa nitashindwa kushiriki tendo la ndoa na mke wangu.

"Sasa nimeamini ni jambo la kawaida, pia linasaidia kutokomeza mimba zisizotarajiwa, hivyo nawashauri wanaume wenzangu kufunga uzazi," anasema Samwel.



Huduma ya uzazi wa mpango ikiendeshwa. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

# Bingwa Dk. Mngumi na darasa la unywaji sahihi maji yasikudhuru

**Inatoka Uk. 12**

ujumla," anasema.

Kuhusu unywaji maji kwa kiwango kilichopitiliza (overhydration au water intoxication), Dk. Mngumi anasema, hutokea mtu anapokunywa kiasi kikubwa cha maji kwa muda mfupi, mwili hauwezi kuyatoa au kuyasawazisha kwa njia ya mkojo.

Hapo anataja kiwango sahihi kwa watu wazima ni kunywa zaidi ya lita tano kwa siku au zaidi ya lita moja hadi kufika lita na nusu kwa saa kunaweza kuwa hatari kiafya. "Athari kubwa hutokea wakati figo zinashindwa kuchuja maji zaidi ya kiwango 0.8 ya lita (milimita 80) hadi lita moja kwa saa," anatamka na kuughanisdja na ufafanuzi wa ishara za kunywa maji kupitiliza kiwango.

Anataja ishara za unywaji maji kupita kiasi ni; mkojo kupita kiasi na hutoka kila mara, ukiwa mweupe sana.

Tatu; anataja mtu anavimba mwili wake, mikono, miguu au usoni; huku la nne, mtaalamu huyo anasema anakuwa na hali ya kizunguzungu au maumivu ya kichwa, kutokana na kushuka viwango vya madini sodiamu kwenye damu.

La tano, Dk. Mngumi analitaja kuwa, mtu anahisi uchovu wa mwili kwa kuwa mwili unajaa maji kupita kiasi na huathiri utendaji wa seli.

Jambo la sita linaloathiri kunywa maji zaidi ni kuhisi kichefuchefu na kutapika.

Saba, ni mtu kuwa na mawazo ya kuchanganyikiwa, baada ya kupungua kwa sodiamu kwenye damu (hyponatremia) huathiri kazi za ubongo.

**SHIDA UKIPITILIZA KIASI**

Miongoni mwa madhara ya kunywa maji zaidi, bingwa huyo anasema ni maradhi anayoyataja kswa jina 'Hyponatremia' (kiwango kidogo cha sodaimu).

Kuwapo maji mengi, kunapunguza kiwango cha sodiamu kwenye damu, hali inayoweza kusababisha matatizo ya neva na misuli.

Akisema matokeomabaya zaidi ni mtu kupata kifafa au kupoteza fahamu na inaweza kumletea hali ya kuvimba ubongo (Cerebral Edema). Kushuka kwa sodiamu, kunatajwa kitaalamu kunasababisha maji kuingia ndani ya seli za ubongo na hivyo ubongo huvimba.

"Hali hii inaweza kuwa hatari kwa maisha. Kazi za figo kushuka. Figo hufanya kazi kupita kiasi kujaribu kutoa maji mengi, jambo linaloweza kusababisha uchovu wa figo.

"Kushindwa kupumua, maji kupita kiasi yanaweza kujikusanya kwenye mapafu, hali inayosababisha ugumu wa kupumua.

"Madhara kwa moyo. Ujazo wa damu unaongezeka, hivyo moyo hulazimika kufanya kazi zaidi, jambo linaloweza kuleta matatizo ya moyo," anatamka

**KUEPUKA USIPITILIZE**

Dk. Mngumi anasema ziko njia za kufuata kuepuka kunywa maji kupitiliza, ikianzia na kusikiliza mahitaji ya mwili.

"Kunywa maji taratibu: Usinywe maji mengi kwa wakati mmoja, badala yake kunywa mara kwa mara kwa kiasi kidogo.

"Kufuata hisia za kiu: Kunywa maji pale unapohisi kiu badala ya kulazimisha kunywa.

"Kuangalia dalili za 'overhydration': Ikiwa unahisi dalili kama kizunguzungu, maumivu ya kichwa au uvimbe, punguza unywaji maji na tafuta ushauri wa daktari.

"Unywaji maji kupita kiasi ni hatari kwa mwili na unapaswa kusimamiwa kwa uangalifu, ili kuepuka madhara.

"Vilevile, kuna watu kutokana na changamoto za magonjwa mfano ugonjwa wa figo, watashauriwa kupunguza na kunywa maji yasiyozidi lita moja, kwa saa 24," anasema.

Pia, anasema kuna ushauri wa kunyw maji wakati wa mchana zaidi, kwani kuna upotevu na haja ya kuyarudishia mwilini na sio kukesha kunywa maji usiku.

"Unywaji wa maji '0.5 lita (nusu lita) hadio lita tatu kwa mtu wa kawaida, inatosha, labda awe na sababu za kitaalamu au aina ya kazi anayo ifanya ilete uhitaji wa maji zaidi," anamaliza

**Soma zaidi ukurasa 14**

AFYA

UKO LIKIZO YA MWISHO WA MWAKA?

# Rejea kanuni zifuatazo kudhibiti afya yako, vinginevyo ukirejea...

**Na Mwandishi Wetu**

ISHARA ya mwaka kufika ukingoni ni maadhimisho ya Sikukuu ya Krismasi, ambayo kiutamaduni huunganishwa na mwaka mpya, kwani tofauti zao ni mwaka mmoja tu. Hapana shaka hilo limeshatimu kwa 2024!

Kipindi kilichoko huendana na matukio maalum, ikiwamo mapumziko ya mwisho wa mwaka na baadhi yetu nao huchukua likizo kipindi hicho.

Ingawa nchini likizo hiyo haipo rasmi kisheria, lakini kisera ofisi nyingi na hasa za kimataifa, watu huenda kupumzika na baadhi ya wafanyakazi, hupenda kwenda katika mapumziko mafupi.

Pia, nchini kuna baadhi ya jamii kama za mkoa wa Kilimanjaro, watu huenda nyumbani, huku watani wao wakiwadhihaki 'wanaenda kuhesabiwa.'

Huko makwao wanapumzika, kujumuika kijamii na wanaburudika kadri wanavyoweza. Zao lake, kuna jambo kiafya; watu wanaongezeka uzito na imekuwa jambo la kawaida kwa watu wazima wengi.

Kisaikolojia, likizo mbalimbali za msimu zinaweza kushawishi ulaji kupita kiasi, tabia ya kukaa tu na ulaji wa vyakula vyenye kalori nyingi.

Hapo kuna vidokezo kadhaa vya kusaidia kuepuka kuongezeka uzito, wakati wa msimu huo wa likizo.

Uchunguzi unaonesha kwamba, watu wanaokula bila kuzingatia kanuni na miongozo ya lishe, wana uwezekano mkubwa wa kula kupita kiasi na kupata athari katika miili yao.



Mlo uliokamilika 'vigezo na 'masharti' kula kwa tahadhari na kuzingatia kanuni zake. **PICHA ZOTE: MTANDAO**



Sehemu ya vinavyokamilisha mlo 'dessert' ambavyo vikitumika vibaya, huishia kuzalisha madhara.

**MBINU STAHIKI**

Ili kuzuia hali hiyo, inaelezwa mtu ale kwa uangalifu na kupunguza vikwazo, ikiwa ni pamoja na kazi na vifaa vya elektroniki.

Jaribu kutafuna polepole na vizuri, hali inayomwezesha mlaji kutumia kalori kidogo, vilevile mtu anatakiwa kuvuta pumzi kidogo kabla ya kuanza kula.

Ni hali inayotajwa kuleta utulivu wakati wa kula, ikisaidia kuweka mawazo kamili kwenye sahani, badala ya orodha yako ya mambo mengi ya kufanya.

Tafiti kadhaa zinaonesha kuwa wanaojihusisha na mazoea ya kula, kwa uangalifu wana uwezekano mdogo wa kupata uzito mkubwa.

**MLO WA PROTINI**

Milo ya likizo kwa kawaida huwa na wanga nyingi lakini ina protini kidogo.

Hata hivyo, ni muhimu kujumuisha protini kwa kila mlo, kwa kuwa inakuza utimilifu na inaweza kuwa muhimu kwa kudumisha uzito.

Ulaji protini na milo mingine, unatajwa kupunguza ulaji wa kalori kwa kupunguza njaa na hamu ya kula.

Protini, pia inatajwa manufaa yake katika kudhibiti uzito, kwa sababu inaongeza tindikali ya metaboliki yako na viwango vya homoni zinazopunguza hamu ya kula.

Vyanzo vya protini ni pamoja na nyama, kuku, samaki, na baadhi ya vyakula vya mimea kama maharage.

**VYAKULA VYA NYUZI**

Vyakula vyenye nyuzi, vinatajwa katika utaalamu lishe ni kirutubisho muhimu kuchangia shibe ya mlaji.

Baadhi ya tafiti zinaonesha kwamba, ulaji vyakula vya nyuzi, unasadia kupunguza ulaji kalori kwa ujumla, hali inayosaidia kuzuia kuongezeka uzito wakati wa likizo.

Ni bahati mbaya vinatajwa vyakula vingi vya kawaida nyakati za likizo havina kiasi cha kutosha cha nyuzi.

Watu wanashauriwa kujitahidi kula vyakula vyenye nyuzi nyingi, kama vile mboga, matunda, kunde, nafaka zisizokobolewa, karanga na mbegu.

Watu wengi hutumia muda mrefu kupika wakiwa likizo, hali inayosababisha kuongezeka uzito, kwa sababu ni rahisi kuonja au kujaribu.

Kuonja chakula chako inaweza kuwa muhimu, hasa ikiwa unawapikia wengine, lakini kumega kidogo kidogo kunaweza kuwa zaidi ya kiasi.

Mlaji anapaswa pia kuhakikisha, hana njaa wakati wa kupika, kwani ni rahisi akawa mwonjaji ladha kupitiliza.

**DHIBITI KITIMDAMLO (DESSERT)**

Katika safu ya mlo, kuna kinachoitwa kitaalamu kwa jina 'dessert'. Hiyo ni ladha fulani inayokamilisha mlo, mfano kwa mchana na mara nyingi huwa jamii ya sukari, mathalan 'icer cream', juisi au soda.

Wakati wa likizo kama sasa kwa wengi, hiyo inashauriwa kuepukwa au kupunguzwa kadri inavyowezekana, kwani ina mchango wa kutumia sukari ya ziada, ikiendana na kuongezeka uzito mwilini.

Pia, unatajwa mbadala wa kula taratibu, unaomfanya mtu ahisi kisaikolojia anaridhika zaidi na kuna uwezekano mdogo wa kuzidisha ulaji wake.

> Kisaikolojia, likizo mbalimbali za msimu zinaweza kushawishi ulaji kupita kiasi, tabia ya kukaa tu na ulaji wa vyakula vyenye kalori nyingi.



Juisi hupendwa sana na wengi kukamilisha mlo.

**KUTUMIA SAHANI NDOGO**

Karamu zenye chakula cha jioni, zimekuwa za kawaida wakati wa likizo sehemu nyingi, zikiwaleta pamoja ndugu, jamaa, marafiki.

Ni sherehe anayotakiwa mtu fursa kutumia sahani ndogo, inayomsaidia binadamu kiafya. Kinyume chake ni kwamba, mtu anapokula kikubwa, kwa hamasa ya sahani yake kubwa, inaweza kusababisha kula kupita kiasi.

Kwa hivyo, sahani ndogo ni njia rahisi ya kudhibiti kiasi cha chakula au mlo wako.

**EPUKA VILIVYOSINDIKWA**

Vyakula vilivyochakatwa wakati wa mapumziko ya mwisho wa mwaka, kama vile viazi kwenye mikebe huwa havifai sana.

Vyakula hivyo mara nyingi huwa na sukari nyingi na mafuta yasiyofaa, yenye mchango kuathiri uzito wa asili wa binadamu.

Ili kuzuia kuongezeka uzito, mtu anashauriwa kuchagua chakula na apike, kwa hatua zote. Kwa njia hiyo, kuna mchango wa kufuatilia, hata kudhibiti uzito binafsi.

Pia, inashauriwa kwamba, kunapokuwapo nia ya dhati ya kudhibiti uzito huo, inawezekana ikasaidia kujiwekea mipaka na kushikamana na malengo yako kuhusu ulaji bora wa chakula.

Mara nyingi, watu huacha malengo yao baada ya hali hii kutokea. Hata hivyo, ni bora kuendelea na kufanya chaguo bora zaidi wakati ujao unapokula.

Ingawa kuyasimamia malengo yako ya uzani kunaweza kuchosha wakati wa msimu wa likizo, vidokezo na njia nyingi zinaweza kusaidia kuwa na afya njema, furaha, na kuzingatia uzito wakati huu wa mwisho wa mwaka.

Zaidi ya vidokezo vya jumla vya lishe, ni bora mtu akahakikisha anafanya mazoezi ya kutosha kupunguza ulaji vyakula visivyofaa.

Ikiwa ana bidii, anaweza kubaini kwamba hajazuia tu kuongeza uzito bali hata kupunguza uzito wakati wa msimu huu wa sikukuu za mwisho wa mwaka.

**Kwa mujibu wa BBC**





# Watano wadakwa na magunia 15 ya bangi

Na Renatha Msungu, DODOMA

JESHI la Polisi mkoani Dodoma linawashikilia watu watano wakiwamo madereva wawili kwa tuhuma za kusafirisha gunia 15 za bangi.

Gunia hizo zilikamatwa juzi ndani ya basi la kampuni ya New Best line eneo la Stendi ya Mabasi Nanenane lililopo mkoani hapa.

Akizungumza na waandishi wa habari jana Kamanda wa Polisi mkoani hapa, Geoge Katabazi alisema basi hilo lenye namba za usajili T 882 EBS lilikamatwa katika msako unaoendelea kukamata wahalifu wa matukio mbalimbali.

Kamanda Katabazi alisema basi hilo lilikuwa likitokea Tarime kuelekea Dar es Salaam, baada ya kufika Stendi ya Nanenane mkoani hapa, askari waliokuwa doria wakifanya ukaguzi walilitilia mashaka na baada ya kupekua walibaini uwepo wa gunia hizo za bangi ndani ya buti.

Alisema watuhumiwa hao wamefikishwa kituo cha polisi pamoja na basi hilo wakati uchunguzi ukiendelea kutokana na tuhuma za tukio hilo ambalo huleta athari kubwa kwa jamii.

**"Matumizi ya dawa za kulevya aina bangi zina madhara makubwa sana, ndizo husababisha masuala ya ukatili wa kijinsiaikiwemo**

"Matumizi ya dawa za kulevya aina bangi zina madhara makubwa sana, ndizo husababisha masuala ya ukatili wa kijinsia ikiwemo ubakaji,"alisema Kamanda Katabazi.

Alisema watu wanapotumia bangi huchangia kuongezeka kwa uhalifu kwa sababu wanapozivuta huwasababishia kufikiria kufanya uhalifu.

Kadhalika, alitoa rai kwa madereva wa vyombo vya moto kuwa makini na mizigo inayosafarishwa ili kujiweka salama na kazi wanazozifanya. Kamanda Katabazi alisema jeshi hilo linaendelea na msako katika maeneo mbalimbali mkoani hapa, huku likisisitiza wananchi waendelee kutoa ushirikiano kwa jeshi hilo ili kusaidia kukamata uhalifu unaofanywa.

Katika hatua nyingine Jeshi la Polisi limeendelea kusisitiza jamii kusherehekea Sikukuu ya Christmas na Mwaka mpya kwa utulivu bila kufanya vurugu yoyote katika maeneo mbalimbali mkoani hapa.

Alisema jeshi hilo linaendelea na doria katika maeneo tofauti jijini Dodoma ili kuwabaini wahalifu waliopanga kufanya matukio.



Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama nchini Jenerali Jacob Mkunda akisalimiana na Askofu wa Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Central Tanganyika Askofu Dk Dickson Chilongani mara baada ya ibada ya Krismasi jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Wananchi wapewa mbinu kupambana na tembo

Na Thobias Mwanakatwe, MANYONI

WATAALAM kutoka Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (TAWIRI), Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) wameweka kambi katika Pori la Doroto wilayani Manyoni mkoani Singida kuwafundisha wananchi namna ya kukabiliana na wanyama waharibifu aina ya tembo.

Wataalamu hao wameweka kambi hiyo kuanzia juzi ambapo wanawafundisha wananchi jinsi ya kukabiliana na tembo kwa kutega uzio wa mizinga ya nyuki kwenye mapito ya wanyama hao.

Mtaalamu kutoka TAWIRI, Kipemba Ntimwa, alisema kutega mizinga ya nyuki kunasaidia sana kudhibiti tembo waharibifu ambao wamekuwa wakifanya uharibifu mkubwa kwenye mashamba na makazi ya watu mkoani Singida.

"Uzio wa mizinga ya nyuki ni njia ya kuzuia uharibifu mbalimbali ikiwemo wa mazao unaosababishwa na tembo pindi anapofanikiwa kuingia katika mashamba ya watu na pia faida watakayopata wananchi baada ya makundi ya nyuki kuingia katika mzinga pia watapata mazao (asali) yanayotokana na nyuki," alisema.

Revocatus Meney kutoka TAWIRI alisema wananchi wakizingatia utaratibu wa kutega mizinga ya nyuki kwenye mapito tatizo la tembo ambao wamekuwa wakiharibu mashamba na makazi yao litapatiwa ufumbuzi.

Mmoja wa wananchi hao Samson Manga alisema tembo wamekuwa tatizo sana katika Wilaya ya Manyoni kutokana na kuharibu mashamba yao na hivyo kusababisha wakulima kutopata mavuno kabisa.

Kumekuwa na mfululizo wa matukio ya tembo kuvamia makazi ya watu na kubomoa nyumba ambapo Novemba 10, 2024 tembo zaidi ya 56 walivamia Kijiji cha Mkiwa wilayani Ikungi mkoani Singida na kuvunja nyumba nane na kula vyakula majumbani.

Kutokana na tukio hilo wakazi wa kijiji hicho walifunga Barabara Kuu ya Dodoma-Singida hali iliyomlazimu Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi Dk. Pindi Chana, kufika katika kijiji hicho na kuagiza askari wa TAWA kuweka kambi kijijini hapo.

Kwa Mkoa wa Singida wilaya ambazo zinakabiliwa na tatizo la tembo ni Ikungi, Manyoni, Singida na Halmashauri ya Itigi.

# Askofu: Tuwajali wenye uhitaji wakati wa sikukuu

Na Peter Mkwavila, DODOMA

ASKOFU Mkuu wa Kanisa la House of Glory International Church (HGIC), Living Mwambapa, ameziomba taasisi, mashirika ya kidini na watu binafsi kushirikiana na serikali kusaidia makundi ya watu wenye uhitaji kipindi hiki cha Sikukuu ya Krismas na Mwaka Mpya.

Mwambapa alisema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari juu ya umuhimu wa kuwakumbuka watu wenye uhitaji kuwapunguzia ugumu wa maisha.

Alisema jukumu hilo badala ya kuachia serikali ambayo imekuwa ikiwajibika kuhakikisha inawasaidia misaada mbalimbali ni wakati sasa kwa mashirika na taasisi za kidini kushiriki pia katika kuwaangalia watu hao wenye uhitaji kwa jicho la karibu.

"Jukumu la kuwasaidia ni la watu wote na siyo kwa upande wa serikali, hivyo niwaombe wahisani kuwajibika katika kuhakikisha jamii hiyo ya watu wasiojiweza wananufaika kwa kupunguziwa mzigo wa makali ya kwenye sikukuu hizo"alisema

Pia, aliwataka watanzania wanapoelekea kwenye sikukuu hizo kuhakikisha wanajiimarisha kwenye ulinzi wao na mali zao wenyewe ikiwemo kuepuka unywaji wa pombe unaoweza kusababisha ajali.

"Sikukuu hizo naomba zisherehekewe kwa amani na utulivu watanzania wajiepushe na unywaji wa pombe na vyombo vya moto viendeshwe kwa kuzingatia sheria ili kuepukana na ajali zinazosababisha na madereva wazembe kutokana na uwanywaji" alisema.

Aidha kiongozi wa kiroho aliwaomba wazazi na walezi kuelekea kwenye sikukuu hizo kujiwekea akiba ya fedha kwa ajili ya maandalizi ya wanafunzi ambao waliochaguliwa kuanza na elimu ya sekondali na wale wa shule za msingi.

"Niwaombe wazazi wezangu wanapoandaa bajeti kwenye sikukuu hizi za mwisho wa mwaka wakumbuke pia maandalizi ya wanafunzi wanaoanza kidato cha kwanza na wale wa shule ya msingi ambao na wao wanaingia darasa la kwanza na chekechea" alisema.



# Wakulima wa tumbaku wakumbushwa kulipa madeni

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

WAKULIMA wa Tumbaku wa Chama cha Msingi cha Ushirika Lualaje (Lualaje AMCOS) katika Halmashauri ya Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya, wametakiwa kulipa madeni yao kwa wakati, ili kuepuka mali zao kushikiliwa na kupigwa mnada.

Mwenyekiti wa chama hicho, Alberto Kacheza alitoa wito huo juzi kwenye mkutano mkuu wa mwaka uliolenga kupitia taarifa ya mapato na matumizi pamoja na kufanya tathimini ya uzalishaji wa tumbaku na kupanga mikakati ya kuongeza tija.

Kacheza alisema wapo baadhi ya wakulima kwa makusudi wamekuwa wakilimbikiza madeni ya mikopo ya pembejeo hali inayosababisha kupata hati zenye mashaka.

"Tutaanza kuwachukulia hatua wakulima wasiorejesha mikopo, kupitia mkutano huu wakulima wamependekeza walio na madeni na kushidwa kurejesha mali zao kama mashamba yapigwe mnada kulingana na deni husika," alisema Kacheza.

Alisema msimu huu wamejiwekea malengo ya kuongeza uzalishaji kutoka kilo milioni 1.3 mpaka 1.5 kulingana na hali ya hewa pamoja na mahitaji ya soko la zao hilo.

Alisema msimu uliopita wa kilimo kulikuwa na tatizo katika uzalishaji lililotokana na mabadiliko ya tabianchi na hivyo kutofikia malengo ya uzalishaji waliojiwekea.

**Alishauri chama hicho kuwa na mfuko wa pembejeo wa ushirika ambao utakuwa msaada kwa wakulima na kuacha kusubiri ruzuku kutoka serikalini akidai kuwa wakati mwingine huwa ...**

Makamu Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Ushirika wa Wakulima wa Tumbaku Wilaya ya Chunya (CHUTCU), Isaya Hussen aliutaka uongozi wa ushirika huo kuwa na mipango madhubuti ya ukusanyaji wa madeni ili kuepuka baadhi ya wanachama kulimbikiza.

Alishauri chama hicho kuwa na mfuko wa pembejeo wa ushirika ambao utakuwa msaada kwa wakulima na kuacha kusubiri ruzuku kutoka serikalini akidai kuwa wakati mwingine huwa inachelewesha.

Ofisa Tarafa wa Kipembawe, Kassim Salum alisema serikali imetoa maelekezo kwa viongozi wa Amcos kuanza kuwachukulia hatua wakulima walioshindwa kulipa madeni ikiwemo kutaifisha mali zao ili kufidia madeni hayo.

Alisema wapo wakulima kwa makusudi wanakwepa kulipa madeni na kutorosha maroba ya tumbaku kuuza maeneo mengine, hivyo lazima wawajibishwe kwa mali na mashamba yao kupigwa mnada kwa mujibu wa kanuni na sheria zitakavyoelekeza.

Alisema katika kuhakikisha kilimo cha tumbaku kinafanya vizuri wamechukua sampuli za udongo 500 kwa ajili ya kufanya utafiti na aina ya mazao yatakayozalishwa ili kuongeza tija ya uzalishaji wa zao hilo.



Waumini wakifuatilia misa takatifu ya Krismasi iliyofanyika katika kanisa la mtakatifu Petro Oysterbay, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# TAKUKURU yaanza kumulika Uchaguzi Mkuu 2025

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Mbeya imesema itafuatilia mchakato mzima wa Uchaguzi Mkuu wa 2025, ili kudhibiti vitendo vya rushwa na kuhakikisha wanapatikana viongozi wanaostahili.

Aidha, imeviomba vyama vya siasa na wananchi kwa ujumla kutoa taarifa pale watakapoona viashiria vya rushwa kwenye maeneo yao ili vidhibitiwe mapema kabla havijasababisha madhara kwenye mchakato huo.

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Mbeya, Maghela Ndimbo alisema hayo kwenye kikao na viongozi wa vyama vya siasa na wadau wa uchaguzi kilicholenga kufanya tathmini ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na mikakati ya uchaguzi mkuu ujao. Ndimbo alisema katika uchaguzi uliopita wa serikali za mitaa uliofanyika Novemba 27, taasisi hiyo haikupokea kesi yoyote ya rushwa wala taarifa za vitendo hivyo kabla, wakati na baada ya uchaguzi huo na hivyo wanajipanga zaidi kudhibiti vitendo hivyo uchaguzi ujao.

"Pamoja na kampeni yetu ya 'Takukuru rafiki', tunahitaji ushirikiano wa pamoja na wadau ikiwamo vyama vya siasa na wananchi kwa ujumla ili tuweze kufikia malengo yetu ya kutokomeza vitendo vya rushwa," alisema Ndimbo.

Katibu wa Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Mkoa wa Mbeya, Hamad Mbeyale alisema ili kumaliza vitendo vya rushwa TAKUKURU inapaswa kuendelea kutoa elimu juu ya haki pamoja na kuhakikisha hatua kali zinachukuliwa kwa wanaobainika kujihusisha na vitendo hivyo.

Alisema rushwa imekuwa ikisababisha haki za watu kupotelea mikononi mwa wasiostahili haki hiyo na hivyo kusababisha demokrasia kuharibika ndani ya nchi.

Mwenyekiti wa Chama cha ADC, Godfrey Davis alisema elimu ya rushwa inapaswa kuanzia ngazi za shule za msingi ili kutengeneza taifa lenye uzalendo na maadili akieleza kuwa wanayo matumaini na chombo hicho katika utekelezaji wa majukumu yake.

Naye Mwenyekiti wa Maimamu na mjumbe wa Baraza Kuu la Waislamu (BAKWATA) mkoani Mbeya Sheikh Idd Tua alisema rushwa imelaaniwa katika vitabu tukufu na kwamba wanaofanya vitendi hivyo wanakiuka maandiko takatifu, hivyo wanapaswa kuchukuliwa hatua kali za kisheria.

# Vifo vya uzazi Nyanda za Juu Kusini Magharibi vyapungua

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

VIFO vitokanavyo na uzazi vimepungua kwa asilimia 18 katika kipindi cha miaka mitatu katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini Magharibi, hali ambayo imesababishwa na kuboreshwa kwa huduma za afya katika mikoa hiyo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya, Dk. Godlove Mbwanji alibainisha hayo wakati wa kikao cha tathimini ya vifo vitokanavyo na uzazi kwa mama na mtoto kilichofanyika jijini Mbeya kikiwahusisha wadau mbalimbali wa afya.

Alisema kuwa mwaka 2021 kulikuwa na vifo 121 kati ya vizazi hai 100,000 lakini mwaka 2023 vilipungua na kufikia vifo 83 kati ya vizazi hai 100,000

Kikao hicho kililenga kufanya tathimini na kubadilishana uzoefu wa utekelezaji wa njia bora za kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi katika Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Magharibi inayojumuisha mikoa ya Mbeya, Songwe na Rukwa.

Dk. Mbwanji alisema kupungua kwa vifo hivyo ni kutokana na jitihada za uwekezaji uliofanywa na serikali katika uboreshaji wa miundombinu, vifaa tiba vya kisasa pamoja na utendaji kazi bora wa watumishi wa sekta ya afya nchini.

Hivyo, aliwataka viongozi wa hospitali zote za mikoa ya Nyanda za Juu Kusini Magharibi kufanya kazi kwa kuzingatia utu na kujali wanaowaongoza na kuhakikisha wanakuwa chachu ya kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi na watoto wachanga.

"Ni wajibu wetu kuwa viongozi wenye kujali utu kwa watumishi wetu na wao wana wajibu wa kuwajibika kutimiza wajibu wao ili sisi sote kwa pamoja tuweze kupata matokeo mazuri zaidi ya kupunguza vifo hivi," alisema Dk. Mbwanji.

Awali Ofisa Programu ya Uzazi Salama wa Wizara ya Afya, Dk. Ulimbakisye Macdonald alisema ili kufikia lengo la kupunguza vifo vya mama na mtoto ni lazima watumishi kukumbushana juu ya uwajibikaji kila mmoja kwenye eneo lake la kazi ili kuleta tija kwa taifa.

Alisema lengo la serikali ni kuona vifo hivyo havitokei kabisa, hivyo kupitia Idara ya mama na mtoto Wizara ya Afya imeanzisha huduma za kambi ya matibabu ya madaktari wa Rais Samia pamoja na mafunzo ya kazi kwa watumishi wa hospitali, ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora za matibabu.

HABARI ZANZIBAR

# Naibu Spika ataka kudumishwa mila na utamaduni

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

NAIBU Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Mgeni Hassan Juma amesema wakati umefika kwa wananchi kushirikiana na serikali katika kudumisha mila, silka na utamaduni wa Zanzibar ili kukuza biashara ya utalii.

Aliyasema hayo huko Mwanakwerekwe Wilaya ya Mgharibi B Unguja wakati wa uwekaji wa jiwe la msingi la nyumba ya sanaa, ikiwa ni shamrashamra za kutimiza miaka 61 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Alisema azma ya Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi ni kuona vijana wanajiajiri na kukuza uchumi wa nchi kupitia sanaa ya utamaduni.

Aidha, alisema Zanzibar inategemea kwa kiasi kikubwa biashara ya utalii, hivyo ni vyema jamii kuwaandaa vijana wao ili kuitumia nyumba ya sanaa kwa kupata ujuzi.

Alisema maendeleo ya sayansi na teknolojia, imepunguza nguvu ya utamaduni wa Zanzibar lakini serikali inachukuwa juhudi ya kurejesha utamaduni huo wa asili.

Hata hivyo, aliwataka Wazanzibar hususani wasanii kuitumia sanaa kwa kudumisha umoja, mshikamano na kuitambulisha Zanzibar ndani na nje ya nchi.

Mkuu wa Wilaya ya Magharibi B, Hamida Mussa Khamis, alisema kuwepo kwa nyumba ya sanaa ni hatua muhimu ya kuwasaidia wananchi kupata ajira kupitia sanaa mbalimbali, zilizopo nchini.

Alisema mradi huo ni hatua muhimu ya utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020-2025 katika kuimarisha na kujenga miundombinu ya sanaa Zanzibar.

Kamishna wa Idara ya Sanaa Zanzibar, Omar Salum Mohammed alisema, ujenzi wa nyumba ya sanaa Zanzibar, unatarajiwa kuwa wa ghorofa tatu na kugharimu zaidi ya Sh. bilioni tatu.

Nyumba hiyo ya sanaa Mwanakwerekwe inataraijiwa kutoa mafunzo ya fani mbalimbali ikiwemo ya uchoraji, uchongaji, ushonaji, kudarizi na ushoni.

# Askofu asisitiza amani kuelekea uchaguzi mkuu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

ASKOFU wa Kanisa la Katoliki Minara Wiliwili Zanzibar, Augustino Shao, amesema ni vyema kila mtu akalinda amani ya nchi, hususani kuelekea kipindi cha Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025.

Alisema hayo jana katika hotuba yake ya mkesha wa ibada ya Sikukuu ya Krismasi visiwani hapa.

Askofu Augustino alisema amani na utulivu ndiyo mambo ya msingi yanayotakiwa kufanyiwa kazi na kuzingatiwa katika kipindi chote kwa serikali pamoja na viongozi waliopo madarakani.

Alisema amefurahishwa katika kipindi cha miaka minne kwa kushuhudia serikali ikipiga hatua kubwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo na uchumi ambayo ni sehemu ya ukuaji wa uchumi na maendeleo.

**"Huo ndiyo ujumbe wangu mwaka 2024...haki na kudumisha amani inayojenga matumaini kwa wengi" kama ndiyo njia pekee ya kuhakikisha tunaishi katika dunia hii kwa amani na utulivu" alisema.**

Askofu Augustino alisema utekelezaji wa miradi ya aina hiyo inaleta matumaini makubwa kwamba maisha ya wananchi yatakuwa bora.

Hata hivyo, alisisitiza zaidi suala la uwajibikaji kwa watendaji waliokabidhiwa majukumu yao kuona kwamba wanasimamia vizuri majukumu yao kwa mujibu wa sheria.

"Huo ndiyo ujumbe wangu mwaka 2024...haki na kudumisha amani inayojenga matumaini kwa wengi" kama ndiyo njia pekee ya kuhakikisha tunaishi katika dunia hii kwa amani na utulivu" alisema.

Katika hatua nyengine, Askofu wa Kanisa la Anglikana Dk.Philip Baji, alisema Tanzania ni miongoni mwa nchi duniani ambazo zinasifika kwa kuwepo kwa amani na utulivu kwa wananchi wake na hivyo kupata fursa kubwa ya kuleta maendeleo na ukuaji wa uchumi.

Alisisitiza na kutaka amani hiyo kudumishwa wakati taifa likielekea katika uchaguzi mkuu kwa ajili ya kupata viongozi watakaoiongoza nchi katika mikono salama.



Watoto wa kikundi cha Haki na Amani Zanzibar wakiimba kwenye ibada ya mkesha wa Krismas jana.**PICHA: MARTIN KABEMBA**

# SMZ yajivunia uboreshaji huduma za afya, miundombinu

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman amesema Serikali ya Zanzibar inaendelea kuchukua hatua za kuimarisha huduma za afya sambamba na ujenzi wa miundombinu.

Othman ambaye pia ni Mwenyekiti wa Taifa wa ACT- Wazalendo, aliyasema hayo juzi katika Hospitali ya Wilaya ya Wete iliyopo Kinyasini Mkoa wa Kaskazini Pemba akizungumza baada ya kuweka jiwe la msingi la ujenzi wa nyumba za wafanyakazi wa hospitali hiyo.

Alisema kwamba hatua hiyo ya serikali pia inakwenda sambamba na uwekaji wa vifaa vya kisasa vya huduma za afya, ili kuwapatia wananchi wa Zanzibar huduma bora na kuhakikisha upatikanaji wa huduma za matibabu ya dharura.

Alisema serikali inafarijika kuona kwamba inaendelea kusimamia na kuhakikisha watoa huduma za afya wanapatiwa makazi bora, ili kutoa huduma bora kwa wananchi na kueneza ufanisi katika kutekeleza majukumu yao.

Aidha alisema ujenzi wa makazi karibu na hospitali ama vituo vya afya kutasaidia kuwapunguzia masafa na gharama za usafiri wa kuwafuata madaktari bingwa na wafanyakazi wengine jambo linaloimarisha huduma za matibabu ili wananchi wote wapate matibabu kwa wakati.

Hivyo, alitoa wito kwa Wizara ya Afya kuanza kufikiria namna bora na utaratibu sahihi wa kuzitunza nyumba hizo kwa kuzingatia kuwepo mpango wa kuzikarabati kwa wakati.

Pia, aliwataka wananchi kuendelea kutoa ushirikiano kwa kuitumia hospitali hiyo ipasavyo kwa kufanya uchunguzi wa maradhi kwa kufuata utaratibu wa rufaa wa matibabu kwa mujibu wa miongozo iliyowekwa.

Othman alieleza umuhimuwa wananchi kujikinga na maradhi mbalimbali akisema kinga ni bora kuliko tiba na kwamba kufanya hivyo kutaipunguzia serikali mzigo wa gharama za kuwatibu wananchi.

Pia aliuagiza uongozi wa Mkoa wa Kaskazini Pemba kushirikiana na Wizara ya Afya kuhakikisha kipande cha barabara inayoingia hospitali hiyo kutoka eneo la Barabara Kuu ya Kinyasini hadi hospitali hapo inajengwa ili kuondoa usumbufu kwa wagonjwa.

Waziri wa Afya, Nassor Ahmed Mazurui alisema kwamba dhamira ya wizara hiyo ni kuhakikisa upatikanaji wa huduma bora za afya kwa wananchi na pia kupunguza vifo vya mama na mtoto kwa kutengeneza mazingira mazuri ya utoaji huduma kwa umma.

Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba, Salama Mbarouk Khatib alisema kwamba ujenzi wa nyumba hizo ni sehemu ya kuendeleza miradi ya maendeleo, kutimiza lengo la mapinduzi.

Alisema kwamba mwaka huu jumla ya miradi 16 itawekewa mawe ya msingi, kuzinduliwa.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya Zanzibar, Miraji Mzee Mgereza alisema kwamba mradi huo hadi utakapokamilika utagharimu Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Sh. bilioni 4.1 na utaondoa usumbufu kwa madaktari na wafanyakazi wengine katika hospitali hiyo.

# HABARI PICHA



Waumini wa Kanisa Katoliki la Kristo Mfufuka Mtaa wa Majengo, wilayani Muheza, mkoani Tanga wakitoka kanisani katika ibada ya sikukuu ya Krismasi jana. **PICHA: STEVEN WILLIAM**



Watoto na waumini wa Kanisa la St Alban, wakifanya maigizo wakati wa mkesha wa ibada ya Krismasi jijini Dar es Salaam juzi usiku. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Mkuu wa KKKT na Askofu wa Dayosisi ya Mashariki na Pwani, Dk. Alex Malasusa, akihubiri katika ibada ya sikukuu ya Krismasi kwenye kanisa la Azania Front, jijini Dar es Salaam jana **PICHA: JUMANNE JUMA**



Watoto wakiogelea na kubembea katika eneo la Msekwa Park, wilayani Muheza, Tanga jana katika kusheherekea sikukuu ya Krismasi. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

HABARI KIMATAIFA

## Waandishi wauawa Haiti

**PORT AU PRINCE,** Haiti

WATU watatu wamefariki dunia baada ya wafuasi wa magenge ya uhalifu nchini Haiti kuwafyatulia risasi waandishi wa habari.

Taarifa ya polisi ilisema tukio hilo lilitokea wakati wa mkutano wa kutangaza kufunguliwa tena kwa hospitali kubwa ya umma nchini humo.

Wanahabari wawili na polisi waliripotiwa kuuawa kwa kupigwa risasi, huku wengine wakijeruhiwa katika shambulio hilo lililofanyika juzi katika hospitali hiyo iliyoko katika mji mkuu wa Port-au-Prince.

Kituo hicho cha matibabu kilirudishwa tena katika mikono ya serikali ya Haiti mnamo Julai, baada ya kukaliwa na kuharibiwa na magenge hayo.

Muungano wa genge la Viv Ansanm, ambalo linadhibiti sehemu kubwa ya jiji, limekiri kutekeleza shambulio hilo.

Picha zilizochapishwa mtandaoni zinaonesha watu kadhaa wakiwa wamejeruhiwa na wengine wakiwa wamefariki ndani ya jengo hilo.

Wanahabari walikuwa wakisubiri kuwasili kwa Waziri wa Afya, Lorthe Blema, ndipo ufyatuaji risasi ulipoanza.

Msemaji wa Online Media Collective, Robest Dimanche, alisema waandishi Markenzy Nathoux na Jimmy Jean waliuawa papo hapo wakati wa shambulio hilo.

Aliongeza kuwa waandishi wengine wa habari walijeruhiwa.

"Ilionekana kama sinema mbaya," alisema Dieugo André, mpigapicha ambaye alishuhudia vurugu hizo.

Aliongeza "Nina damu ya waandishi wa habari kadhaa waliojeruhiwa kwenye nguo zangu."

Katika video ya mtandaoni inayodai shambulio hilo, muungano wa genge la Viv Ansanm, ulisema haujaidhinisha kufunguliwa tena kwa hospitali hiyo, ambayo waliikalia.

Mkuu wa baraza la mpito la rais wa Haiti, Leslie Voltaire, alitoa pole kwa familia zote za wahasiriwa, haswa kwa Polisi wa Haiti na vyama vyote vya waandishi wa habari. **BBC**

# Mondlane kujiapisha urais wa Msumbuji

**MAPUTO,** Msumbiji

KIONGOZI wa upinzani nchini Msumbiji, Venancio Mondlane, ametangaza Januari 15, mwakani atajiapisha kuwa rais wa Msumbiji.

Alitoa tangazo hilo jana baada ya kukataa matokeo ya uchaguzi wa urais yaliyompa ushindi mgombea wa chama cha Frelimo.

Hata hivyo, baada ya mahakama kuthibitisha matokeo hayo, wafuasi wake waliingia barabarani kufanya maandamano yaliyoambatana na ghasia nchini kote wakitaka kumalizika kwa utawala wa miaka 49 wa chama cha Frelimo.

Mitaa ya mji mkuu wa Maputo ilikuwa vururgu tupu usiku wa mkesha wa Krismasi, na biashara zote zimefungwa kuhofia ghasia

Aidha, ofisi za Frelimo, vituo vya polisi, benki na viwanda vimeporwa na kuharibiwa kwa kuchomwa moto.

Waziri wa Mambo ya Ndani wa Msumbiji, alisema tangu kuanza kwa ghasia hizo Jumatatu, watu 21 wameuawa katika machafuko hayo.

Waziri Pascoal Ronda, aliwaambia waandishi wa habari juzi jioni kwamba jumla ya matukio 236 ya vurugu yaliripotiwa nchini kote na kusababisha watu 25 kujeruhiwa wakiwamo polisi 13.

Alisema makundi ya watu wenye silaha wameshambulia vituo vya polisi, magereza na miundombinu mingine na kwamba hadi sasa zaidi ya watu 70 wamekamatwa.

Mahakama ya juu ya taifa hilo ilithibitisha ushindi wa chama cha Frelimo ambacho kipo madarakani tangu mwaka 1975.

**BBC**



Waandamanaji wakichoma matairi barabarani katika maandamano yaliyoambatana na vurugu mjini Maputo juzi. **PICHA: AFP**

## Russia yashambulia alikozaliwa Zelensky

**KYIV,** Ukraine

MTU mmoja ameuawa na wengine zaidi ya 12 wamejeruhiwa kufuatia mashambulizi ya makombora yaliyofanywa na Russia kwenye mji wa kusini-mashariki mwa Ukraine wa Kryvyi Rih.

Hata hivyo, mwanamke mmoja aliokolewa akiwa hai kutoka kwenye vifusi vya nyumba iliyoharibiwa na shambulio hilo.

Mkuu wa jeshi wa eneo hilo, Oleksandr Vilkul, alisema shambulio hilo lilipiga jengo la makazi katika mji huo wenye watu 600,000.

Mkuu wa ofisi ya Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelensky, Andriy Yermak, alichapisha nyumba iliyoharibiwa katika mtandao wa Telegram na kuongeza kuwa, kufikia jana jioni, idadi ya majeruhi ilikuwa 15.

Kryvyi Rih, mji alikozaliwa Rais Volodymyr Zelensky, umekuwa ukishambuliwa mara kwa mara na makombora na ndege zisizokuwa na rubani. **DW**

## Denmark yaongeza ulinzi kisiwa cha Greenland

**KOPENHAGEN,** Denmark

DENMARK imetangaza kuimarisha ulinzi katika kisiwa cha Greenland, baada ya Rais mteule wa Marekani Donald Trump, kueleza anataka kulinunua eneo la Arctic.

Waziri wa Ulinzi wa Denmark Troels Lund Poulsen alisema serikali imeongeza pesa ya kuimarisha ulinzi hadi kufikia dola bilioni 1.5.

Alielezea tangazo la Trump kama kitendo cha kejeli.

Jumatatu Trump alisema lazima umiliki na udhibiti wa kisiwa hicho kikubwa uwe chini ya Marekani.

Greenland, eneo linalojiendesha la Denmark, ni nyumbani kwa kituo kikubwa cha anga za juu cha Marekani na ni muhimu kimkakati kwa taifa hilo ikiwa ni njia fupi zaidi kutoka Amerika Kaskazini hadi Ulaya.

Kisiwa hicho kina hifadhi kubwa ya madini.

Poulsen alisema gharama hiyo itaruhusu ununuzi wa meli mbili mpya za ukaguzi, ndege mbili mpya zisizo na rubani na za masafa marefu na timu mbili za ziada za mbwa.

Pia itajumuisha ufadhili wa kuongeza wanajeshi katika kambi ya kijeshi ya Arctic katika mji mkuu wa Nuuk na uboreshaji wa viwanja vya ndege vitatu vya kiraia vya Greenland ili kushughulikia ndege za kivita za F-35.

"Hatujawekeza vya kutosha katika Arctic kwa miaka mingi, sasa tunapanga uwepo wa nguvu zaidi," alisema.

Waziri wa ulinzi hakutoa kiwango cha ufadhili huo, lakini vyombo vya habari vya Denmark vilikadiria kuwa karibu krone bilioni 12-15.

Tangazo hilo limekuja siku moja baada ya Trump kusema kwenye jukwaa lake la mtandao wa kijamii la Truth Social kwamba madhumuni ya usalama wa Taifa na Uhuru Duniani, Marekani inahisi kuwa mmiliki na mdhibiti wa Greenland ni jambo la lazima kabisa.
**BBC**

HABARI MICHEZO

# STRAIKA SINGIDA BS HASHIKIKI KUPACHIKA MABAO LIGI BARA

Na Adam Fungamwango

STRAIKA wa Singida Black Stars, Elvis Rupia, ameendelea kuonesha uhodari wake wa kucheka na nyavu baada ya kufikisha mabao manane na kukaa kileleni katika orodha ya wafungaji katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara inayoendelea hapa nchini.

Rupia alifunga bao moja katika ushindi wa mabao 2-1 wakati timu yake ilipocheza dhidi ya KenGold katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa juzi.

Taarifa za ndani zinasema vinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba wameanza kumwinda straika huyo raia wa Kenya ili kumsajili kipindi hiki cha dirisha dogo la usajili.

**Rupia aliingia kipindi cha pili katika mechi hiyo iliyochezwa kwenye Uwanja wa Liti mkoani, Singida na kupachika bao lililowapa ushindi timu yake huku mwenyewe akisema kila akiingia uwanjani huwa na malengo ya kufunga angalau bao moja.**

"Kila nikiingia uwanjani malengo yangu ni kufunga bao moja tu, wala sitaki zaidi, sasa nikitoka bila kufunga hiyo ni bahati mbaya, na nikifunga mawili kama ilivyokuwa kwenye mchezo uliopita dhidi ya Prisons inakuwa kama bonasi tu, ila nashukuru sana kwa kufika hapa, siri ni kujituma kwenye mazoezi na kujiwekea malengo kama haya," Rupia alisema.

Straika huyo anafuatiwa kwa karibu na kiungo mshambuliaji wa Simba, Jean Ahoua, ambaye baada ya kufunga bao pekee kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam dhidi ya JKT Tanzania juzi, amefikisha mabao saba.

Straika ambaye kwa muda mrefu alikuwa akiongoza kwenye jedwali la wafungaji, Selemani Mwalimu wa Fountain Gate, ana magoli sita akiwa kwenye nafasi ya tatu, huku nafasi ya nne ikichukuliwa na wachezaji waliofunga mabao matano kila mmoja ambao ni Leonel Ateba wa Simba, Edgar William ( Fountain Gate) na Peter Lwasa wa Kagera Sugar.

Wachezaji wenye mabao manne ni Feisal Salum wa Azam FC, Yacouba Songne (Tabora United), Marouf Tchakei ( Singida Black Stars) na Ibrahim Hamad 'Bacca', Prince Dube, wa Yanga, kabla ya mchezo wao dhidi ya Dodoma Jiji uliochezwa jana jioni.



Wachezaji wa Timu ya Soka ya Taifa ya vijana wa umri chini ya miaka 17 (Serengeti Boys), wakishangilia baada ya kukata tiketi ya kushiriki Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON U-17) baada ya kuifunga Sudan Kusini mabao 4-0 katika mechi ya hatua ya nusu fainali ya Ukanda ya CECAFA iliyochezwa kwenye Uwanja wa Nakivubo jijini Kampala, Uganda juzi. **PICHA: TFF**

# Mandonga : Nitamchapa Mbelwa

Na Shufaa Lyimo

BONDIA Karim Mandonga anatarajiwa kupambana na Said Mbelwa katika pambano la Boxing on Boxing Day litakalofanyika leo kwenye Uwanja wa Zimbihile ulioko mkoani, Kagera imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mandonga alisema amejipanga vyema kumtwanga mpinzani wake huyo kwa sababu amefanya mazoezi ya kutosha.

Bondia huyo amesema amefanya maandalizi kwa muda mrefu na ya kiwango cha juu na amepanga ushindi atakaopata utakuwa ni zawadi kwa Rais Samia Suluhu Hassan.

"Kwa upande wangu nimejipanga vizuri kuhakikisha ninamtwanga mpinzani wangu nataka nifunge mwaka kwa furaha," alisema Mandonga.

Aliongeza pia kutakuwa na pambano la wanawake ambalo litawakutanisha, Hidaya Zahoro kutoka Morogoro dhidi ya Maria Mungi wa Dar es Salaam huku Ayubu Mwankina wa Morogoro atapambana na Reagen Pacho kutoka Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DR Congo) wakati Abdallah Pazi maarufu Dula Mbabe atachuana na Mada Maugo.

Kwa upande wake, Hidaya alisema hana wasiwasi kukutana na Maria kwa sababu amemfuatilia kwa muda mrefu kufahamu uwezo wake.

"Huyu hanipi shida ninamjua vizuri, ninafahamu sehemu gani ya kumpiga, ninaomba mashabiki wangu waje kwa wingi kushuhudia kipigo," alisema Hidaya.

# TRA, BASATA mifumo ya kodi sasa kusomana

Na Pilly Kigome

BARAZA la Sanaa la Taifa (BASATA) limeingia makubaliano na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ya kubadilishana taarifa, kusomana mifumo ya kudhibiti mapato yatokanayo na wasanii na kubaini wasanii wanaolipa kodi na wasiolipa kodi.

Kamishna Mkuu wa (TRA), Yusuphu Mwenda, alisema jijini jana, makubaliano hayo yatawezesha kusomana mifumo kati ya TRA na BASATA katika ukuzaji na kuendeleza sekta ya saana nchini.

Mwenda alisema hiyo ni katika utekelezaji wa agizo la Rais, Samia Suluhu Hassan, kutaka taasisi, makampuni ya umma kusomana kwa mifumo na taarifa.

Alisema mifumo hiyo itaweza kubaini na kutambua ni wasanii gani na wangapi wamesajili na TRA na kujua ambao hawajasajiliwa ili waweze kuwasaidia kutambulika kuwasajili na kupata TIN namba kwa gharama kidogo.

Aliongeza makubaliano hayo yatalenga kuwapa mafunzo wasanii wote ili wawe mabalozi wa TRA kwa sababu wanakutana na watu mbalimbali wakiwamo Ma-MC, wasanii ili na wao waweze kuchangia pato la taifa kutokana na shughuli zao zao kila siku.

"Msaniii atakayekuwa na mapato ya chini ya Sh. 170,000 Serikali imemsamehe, atakayekuwa mapato yatakayozidi hapo atachangia kiasi kidogo, msanii atakayeanzisha kampuni yake akiwa na mapato chini ya Sh. milioni nne kwa mwezi atasamehewa kulipa kodi lakini akiwa na mapato kwa mwaka kuanzia Sh. miliomi saba atachangia Sh. 100,000 kwa mwezi.

Yule ambaye atakayekuwa na mapato ya kuanzia Sh. milioni saba hadi Sh. milioni 11 atalipa Sh. 250,000 na akiwa na mapato kuanzia Sh. milioni 11 hadi Sh. milioni 100 kwa mwezi atachangia asilimia tatu na nusu ya kile anachoingiza," bosi huyo.

Naye Katibu Mtendaji BASATA, Dk. Kedmon Mapana, alisema mifumo itasaidia kuleta mapinduzi na mabadiliko makubwa katika sekta ya sanaa kwa wasanii wote wakiwamo waimbaji, wachoraji, MC.

"Kwa ujumla huu mchakato utawahusu wasanii wote, bila kuwasahau wachongaji na wengine wote wataingia kwenye kundi hilo," Mapama alisema.

Aliongeza TRA inakwenda kuipa Serikali mwamko ya kuisaidia sekta hii kufuatia wasanii watakaolipa kodi itakwenda kuwagusa wadau wa sanaa kufanya shughuli zao bila bughudha yoyote kufuatia kusomana kwa mifumo.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

**OSIMHEN AKARIBIA UNITED**

KLABU ya Manchester United imepewa nafasi ya kumsajili mshambuliaji wa Nigeria, Victor Osimhen,katika dirisha la Januari, huku Napoli wakiwa tayari kwa mkataba wa kubadilishana wachezaji kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, ambaye kwa sasa yuko kwa mkopo Galatasaray. (***TBR Football***)

**PICKFORD SAFI EVERTON**

EVERTON inajiandaa kumpa kipa wa Timu ya Taifa ya England, Jordan Pickford, ambaye ana umri wa miaka 30, mkataba mpya ambao utamweka katika klabu hiyo kwa maisha yake yote yaliyosalia. (***TBR Football***)

**CUYPER NYOTA IMENG'AA**

CHELSEA, Arsenal na Tottenham Hotspur zote zimetuma maskauti kumtazama beki wa pembeni wa Club Brugge na Timu ya Taifa ya Ubelgiji, Maxim de Cuyper, mwenye umri wa miaka 24. (***Caughtoffside***)

**OYEDEJI ATAKIWA ZURICH**

FC Zurich imewasiliana na Arsenal kuuliza kuhusu upatikanaji wa mshambuliaji wa England, Nathan Butler-Oyedeji, mwenye umri wa miaka 21 dirisha la Januari litakalofunguliwa. (***Football Insider***)

**MUAMI KUTUA ARSENAL**

KLABU ya Paris St-Germain huenda ikaipa Arsenal nafasi ya kumsajili fowadi wao, Randal Kolo Muani, mwenye umri wa miaka 26. (***Standard***)

**CALDERON ANUKIA ROVERS**

BOSI wa Brighton, Inigo Calderon, mwenye umri wa miaka 42, yuko kwenye mazungumzo ya juu ili kuwa kocha mpya wa Bristol Rovers. (***Sky Sports***)

**BAYERN YAMTAKA WIRTZ**

KLABU ya Bayern Munich ina matumaini ya kutaka kumnunua kiungo mshambuliaji wa Ujerumani, Florian Wirtz, mwenye umri wa miaka 21, ambaye yuko kwenye majadiliano na Bayer Leverkusen kuhusu mkataba mpya. (***Sky Germany***)

**UNITED NA NISTELROOY**

KOCHA wa Leicester City, Ruud van Nistelrooy, anaweza kuegemea kwenye uhusiano wake na Manchester United ili kupata wachezaji wa mkopo watakaomsaidia ifikapo Januari. (***Football Insider***)

**UNITED ILIJIPANGA MAPEMA**

KLABU ya Manchester United ilianza kutafuta mrithi wa muda mrefu wa Erik ten Hag mara tu kocha wao wa zamani alipotia saini mkataba mpya msimu wa joto. (***Telegraph***)

**AKLIOUCHE AITAKA BARCA**

KIUNGO mshambuliaji wa Monaco na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Maghnes Akliouche, mwenye umri wa miaka 22 amesema angependa kuichezea Barcelona katika maisha yake ya soka. (***Sport***)

**NELSON MAMBO SAFI**

WINGA wa Arsenal, Reiss Nelson, ambaye kwa sasa yuko kwa mkopo Fulham ataruhusiwa kuondoka kwa washikabunduki hao msimu ujao kutokana na uwezekano mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 hatakuwa sehemu kubwa ya mipango ya Mikel Arteta katika siku zijazo. (***Mail Plus***)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# AMORIM AFUNGUKA KUHUSU RASHFORD

## Asema mshambuliaji huyo anatakiwa kubadilika ili arejee katika...

**MANCHESTER,** England

RUBEN Amorim amemwonya, Marcus Rashford, endapo ataendelea kuachwa katika kikosi chake hadi atakapoanza kufikia viwango vinavyotakiwa kwa mchezaji wa Manchester United.

**Rashford ameondolewa katika kikosi cha timu hiyo kwenye mechi tatu zilizopita ambazo zilikuwa ni dhidi ya Manchester City, Tottenham Hotspur na Bournemouth.**

Amorim amesema kuachwa kwake kunatokana na kiwango duni mazoezini baada ya mahojiano ambayo Rashford alisema anataka kuondoka katika klabu hiyo, na kocha huyo alibainisha ataendelea kumwacha mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 hadi atakapojirekebisha.

"Ninapohisi ni wakati mwafaka nitabadilisha kitu, lakini kwa sasa nitaendelea kufikiria ni nini bora kwa timu," alisema Amorim alipoulizwa kuhusu hali ya Rashford.

"Ninazungumza naye kila siku, sio kuhusu mahojiano lakini kuhusu uchezaji.

"Ni uamuzi wangu. Anataka kucheza. Anajaribu. Ni uamuzi wangu, uamuzi wangu tu. Ninajaribu kufanya mambo kwa njia yangu. Na ndio njia pekee ninayojua nisipofanya hivyo nitapoteza mwenyewe na sitajipoteza najua ninachofanya."

Baada ya kufungwa mfululizo na Tottenham na Bournemouth, United itacheza mechi nyingine ya Ligi Kuu England leo dhidi ya Wolves.

Alipoulizwa ni nini Rashford anahitaji kufanya kabla ya kufikiria kurejea kwenye uwanja wa mazoezi wa Molineux, Amorim alijibu: "Kuwa bora zaidi awezavyo kuwa.

"Ikiwa huna vipaji vikubwa, utendaji mkubwa, jukumu kubwa, ushiriki mkubwa, songa mbele. Na baadhi ya watu wana jukumu kubwa hapa kwa sababu wako hapa kwa muda mrefu."

# GUARDIOLA ATAKA SASA CITY IMSAIDIE HAALAND




**MANCHSTER,** England

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, amemtetea mshambuliaji nyota, Erling Haaland na kusema ni lazima timu "imtumie vyema" ili kumsaidia kurudisha kiwango chake kilichoshuka.

Wakati Haaland bado yuko katika nafasi ya pili kwenye safu ya ufungaji mabao ya Ligi Kuu England akiwa na mabao 13 msimu huu, amefunga mara nne pekee katika mechi zake 13 zilizopita.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, kushuka kwake kwa kiwango kumeambatana na matatizo ya City kama timu.

Kikosi cha Guardiola kimeporomoka hadi nafasi ya saba katika msimamo wa Ligi Kuu England kwa kushinda mara moja katika mechi nane zilizopita.

Lakini kocha huyo alimtetea Haaland akisema lazima wamtumie vyema ili kurejea katika mstari.

"Inatuhusu, sio mchezaji mmoja tu. Wakati Erling alikuwa hodari sana, ilituhusu sisi kama timu," alisema Guardiola katika mkutano wa waandishi wa habari kuelekea mechi ya City dhidi ya Everton itakayochezwa leo.

"Erling ni muhimu sana kwetu na atakuwa muhimu sana kwetu. Tunahitaji kumtumia vyema zaidi.

"Sababu inatuhusu sisi, kuhusu kila mtu."

# Van Dijk: Sijui chochote kuhusu mkataba



**LIVERPOOL,** England

VIRGIL van Dijk amekataa kuweka muda maalumu wa mazungumzo ya mkataba wake na Liverpool, lakini alikiri bado hakuna chochote kuhusu mustakabali wake na klabu hiyo.

Van Dijk anakaribia miezi sita ya mwisho ya mkataba wake na tayari amekataa ofa ya awali ya Liverpool ya kuongeza muda, huku masharti yaliyopo mezani hayaridhishi kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33.

Inamaanisha Mholanzi huyo amesalia siku chache tu ili aweze kuzungumza na klabu nyingine.

Licha ya ukweli muda unakwenda, Van Dijk alisisitiza hataweka muda kuhusu uamuzi wake.

Akithibitisha hakuna taarifa kuhusu hali yake, Van Dijk aliwaambia waandishi wa habari: "Hakuna tarehe ya mwisho kabisa. Tutaona nini kitaleta siku zijazo."

Van Dijk alisisitiza tena umakini wake unabaki kwenye masuala ya uwanjani tu, akianza mechi ya leo kati ya Liverpool dhidi ya Leicester City.

"Nazingatia mchezo dhidi ya Leicester," alisema nyota huyo.

Mabadiliko ya mkataba wa Van Dijk yanakuja muda mfupi baada ya Mohamed Salah pia kuthibitisha hakuna jipya la kusema kuhusu mazungumzo yake ya kuongeza muda.

# Osimhen kumrithi Marcus United

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United inawasiliana na wawakilishi wa mshambuliaji wa Napoli, Victor Osimhen huku wakiangalia uwezekano wa yeye kuchukua nafasi ya Marcus Rashford, kwa mjibu wa ESPN.

Rashford yuko katika hali mbaya baada ya kukiri hadharani nia yake ya "changamoto mpya" baada ya uamuzi wa kocha mpya, Ruben Amorim, kumwondoa katika kikosi cha United katika mechi dhidi ya Manchester City.

Tangu wakati huo ameondolewa kwenye vikosi vingine viwili vya mechi.

Mshahara wa Rashford ni zaidi ya pauni 300,000 kwa wiki - ripoti zinaonyesha United wanahitaji kuondoa mshahara huo kabla ya kutafuta mbadala wake.

Kwa mujibu wa ESPN, maofisa wa United wanampanga, Osimhen, kama mbadala anayetarajiwa na tayari wanawasiliana na wawakilishi wa mshambuliaji huyo.

Osimhen alijiunga na Galatasaray kwa mkopo kutoka Napoli wakati wa majira ya joto baada uhamisho wa kwenda Chelsea kushindikana, lakini timu hiyo ya Serie A inaaminika wana chaguo la kumuuza Januari ikiwa watapata ofa nzuri.

Napoli inataka ada ya takribani euro milioni 75 ili kumuuza Osimhen, ambaye amebakiza miezi 18 kwenye mkataba wake na tayari amewaarifu muda wake katika klabu hiyo umekwisha.

Ada hiyo inatarajiwa ni ya juu sana kwa United, kwa sababu Rashford amethaminiwa kuuzwa kwa pauni milioni 40.



## JKT Tanzania yalia refa amewamaliza

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa JKT Tanzania, Hamad Ally, amesema hajafurahishwa na matokeo waliyoyapata katika mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Simba iliyochezwa juzi na kuahidi kujipanga vyema kwa ajili ya mzunguko wa pili wa ligi hiyo.

Simba ikiwa mwenyeji wa mechi hiyo ya kiporo ilipata ushindi wa bao 1-0, Jean Ahoua, akifunga kwa penalti dakika za lala salama.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ally alisema aliwaandaa vyema wachezaji wake isipokuwa bahati haikuwa upande wao na kuwataka mashabiki wasikatishwe tamaa.

"Malengo yalikuwa ni kumaliza mzunguko huu kwa ushindi, isipokuwa imekuwa tofauti, kilichobaki kwa sasa tunakwenda kujipanga kwa ajili ya mzunguko wa pili ili tumaliza katika nafasi za juu katika msimamo wa ligi," alisema Ally.

Kocha huyo alisema licha ya kupoteza mchezo huo hajakata tamaa kwa sababu anakwenda kufanyia kazi mapungufu aliyoyabaini ili wafanye vizuri kwenye mzunguko wa pili ambao ndio unafunga hesabu za msimu.

Naye Ofisa Habari wa JKT Tanzania, Masau Bwire, alisema hajaridhishwa na ushindi walioupata Wekundu wa Msimbazi kwa kueleza mwamuzi wa mchezo huo hakuwatendea haki.

"Sijaridhishwa na maamuzi yaliyofanywa na mwamuzi wa mchezo huu mpaka kutufanya tupoteze mchezo wetu wa leo (juzi)," alisema Bwire.

Matokeo hayo yameifanya Simba kufikisha pointi 37 na kuendelea kujiimarisha katika msimamo wa Ligi Kuu Bara huku JKT Tanzania yenye pointi 19 ikiwa katika nafasi ya nane baada ya kukamilisha michezo yake ya mzunguko wa kwanza.

Kagera Sugar yenye pointi 11 sawa na Tanzania Prisons na KenGold yenye pointi sita zinazubura mkia kwenye msimamo wa ligi hiyo yenye timu 16.

Ligi Kuu Bara inatarajia kuendelea tena leo kwa Azam FC kuwakaribisha JKT Tanzania kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

# AHOUA, FEI TOTO, HATARI MAGOLI YA PENALTI BARA

**Na Adam Fungamwango**

KIUNGO mshambuliaji wa Simba, Jean Ahoua na Feisal Salum 'Fei Toto' wa Azam FC, wanaongoza kwa kufunga mabao ya penalti katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu inayoendelea.

Wachezaji hao wamefunga mabao matatu kwa njia hiyo, wakiwa hawajapoteza hata penalti moja waliyopewa dhamana ya kupiga.

Ahoua alitimiza bao la tatu kwa njia ya tuta alipofunga na kuipa Simba ushindi wa bao pekee katika mechi dhidi ya JKT Tanzania iliyochezwa kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam juzi.

"Hii siyo ya kwangu peke yangu, ni ushindi wa timu nzima, kila mmoja amechangia kupata ushindi, nafikiri tufurahi leo (juzi), tumepata pointi tatu, tutaangalia mechi ijayo," alisema Ahoua.

Rekodi za dawati la michezo Nipashe zinaonyesha kiungo mshambuliaji huyo ambaye ni raia wa Ivory Coast, alifunga mabao mengine ya penalti dhidi ya Dodoma Jiji, Simba ikishinda pia bao 1-0, nyingine dhidi ya KMC, akiiwezesha timu yake kushinda mabao 4-0.

**Kwa upande wa Fei Toto, penalti zake alizifunga katika mchezo kati ya Azam FC dhidi ya Ken Gold, ikishinda mabao 4-1, dhidi ya Kagera Sugar ikiipa timu yake ushindi wa bao 1-0, na dhidi ya Dodoma Jiji, Wanalam balamba wakishinda mabao 3-1.**



Winga wa Simba, Ladack Chasambi (kulia), akiwania mpira dhidi ya mchezaji wa JKT Tanzania FC, Najim Magulu, katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam juzi. Simba ilipata ushindi wa bao 1-0. **PICHA: SIMBA SC**

Wachezaji wanaofuatia kwa kufunga mabao mengi ya penalti ni, Leonel Ateba wa Simba, Erasto Nyoni wa Namungo na Morice Chukwu wa Tabora United.

Ateba alifunga katika mechi ambayo Simba ilitoka sare ya mabao 2-2 dhidi ya Coastal Union, na Pamba Jiji likiwa ni bao pekee kwenye mchezo huo.

Morice alifunga penalti zake kwenye mchezo ambao Tabora United ilishinda bao 1-0 dhidi ya Pamba Jiji na dhidi ya Mashujaa, ikishinda pia bao 1-0.

Wakati huo huo, Fei Toto ndiye kinara wa 'asisti' mpaka sasa kwenye Ligi Kuu, akiwa ametoa pasi saba za mwisho.

Kiungo mshambuliaji huyo anafuatiwa na Salum Kihimbwa wa Fountain Gate FC ambaye ana 'asisti' tano, huku Ahoua, Josephat Bada wa Singida Black Stars wote wakiwa na 'asisti' nne, pamoja na Stephane Aziz Ki, ambaye kabla ya mchezo wa jana kati ya Yanga dhidi ya Dodoma Jiji naye alikuwa na idadi hiyo ya pasi za mabao.



Ligi Kuu Bara inatarajia kuendelea tena leo kwa Tanzania Prisons dhidi ya Pamba Jiji itakayochezwa kwenye Uwanja wa CCM Sokoine jijini, Mbeya huku kesho Azam FC ikiwaalika JKT Tanzania.

# Nane zasonga mbele ZFF Cup

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

JUMLA ya timu nane tayari zimefanikiwa kutinga hatua ya 32 Bora ya mashindano ya Kombe la Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF Cup) inayoendelea visiwani hapa.

Timu hizo ni pamoja na Union Ring, Super Star, Taifa Jang'ombe , Zafsa FC, Urafiki SC, Negro United, Sharp Boys na Kikungwi Star.

Hatua ya awali ya mashindano hayo ilishirikisha timu kutoka Ligi za mikoa mitatu ya Unguja na Ligi Daraja la Kwanza (Unguja).

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu wa Kamati ya Mashindano ya ZFF, Ali Bakari 'Cheupe', alisema ratiba ya mzunguko huo wa kwanza inatarajiwa kukamilika kesho kwa kupata timu 20 zitakazotinga hatua ya 32 Bora.

Bakati alisema katika kuhakikisha mzunguko wa pili unakuwa na mafanikio makubwa, kamati yake inaendelea na jitihada za kutafuta wadhamini ili kusaidia michuano hiyo kuwa na ushindani zaidi.

"Bado hatuna udhamini wa moja kwa moja wa mashindano haya katika hatua ya awali, japo tunaudhamini wa zawadi kwa bingwa tu kutoka katika Benki ya PBZ, hivyo tunawakaribishwa wadau kudhamini mashindano haya," Cheupe alisema.

Mashindano hayo ya FA yanachezwa kwa kanda mbili (Unguja na Pemba) na mshindi wa Kanda ya Unguja atakutana na mshindi kutoka Pemba kupata bingwa ambaye ataiwakilisha Zanzibar katika michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

# Michezo

Alhamisi Desemba 26, 2024

Nipashe





Amorim afunguka kuhusu Rashford UK. 21


# Yanga, Dube moto chini

## ●●● Watoa zawadi safi ya Krismasi kwa mashabiki baada ya kuisulubu...

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA Prince Dube, ambaye ni raia wa Zimbabwe amefikisha mabao matano huku akiiongoza Yanga kuisulubu Dodoma Jiji magoli 4-0 katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara uliochezwa kwenye Uwanja wa Jamhuri Dodoma jijini, Dodoma jana.

**Ulikuwa ni ushindi wa nne mfululizo kwa Yanga, tangu mara ya mwisho ilipofungwa mabao 3-1 dhidi ya Tabora United, mechi iliyofanyika Novemba Mosi, mwaka huu, ambapo baada ya hapo, ili ichapa Namungo FC mabao 2-0, Mashujaa mabao 3-2 na Prisons mabao 4-0.**

Dube amefikisha mabao matano kwa mechi tatu mfululizo alizocheza, akifunga 'ha-trick' katika mechi dhidi ya Mashujaa FC, kwenye ushindi wa mabao 3-2, bao moja dhidi ya Prisons, kabla ya jana kutimiza idadi hiyo ya mabao.

Mabao mengine ya Yanga katika mchezo wa jana yalifungwa na Clement Mzize ambaye amefikisha mabao manne wakati Stephane Aziz Ki, alifunga bao moja.

Ushindi huo umeifanya Yanga kuendelea kung'ang'ania katika nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, lakini ikiendelea kuifukuza Simba kileleni kwa kufikisha pointi 36, ikicheza mechi 14, ikiwa ni pungufu ya pointi moja dhidi ya vinara hao wenye pointi 37.

Aziz Ki, alianza kulitia msukosuko lango ya Dodoma Jiji dakika ya nne, baada ya shuti lake la mbali alilopiga kwa mguu wa kushoto kupita juu kidogo ya mwamba wa lango.

Dakika moja baadaye alifanya jaribio lingine la hatari, baada ya kona aliyopiga kugonga mwamba wa juu, kabla ya kukolewa na mabeki wa Dodoma Jiji.

timu mwenyeji.

Kama ingekuwa makini, Dodoma Jiji ingeweza kujipatia bao dakika ya sita ya mchezo, baada ya mabeki wawili wa Yanga, Ibrahim Hamad 'Bacca' na Nickson Kibabage kugongana wenyewe kwa wenyewe, ikampa nafasi Zidane Sereri kuuchukua kirahisi na kuondoka nao kwenye wingi ya kulia.



Kiungo mshambuliaji wa kimataifa wa Yanga, Stephano Aziz Ki (katikati), akijiandaa kumtoka, beki wa Dodoma Jiji FC, Mkenya Joash Onyango, katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma jana. Yanga ilipata ushindi wa mabao 4-0. **PICHA: YANGA SC**

Hata hivyo, badala ya kumpa mwenzake Idd Kipagwile, aliyekuwa katika nafasi nzuri, aliamua kupiga mwenyewe akiwa kwenye 'engo' ngumu, mpira ukapiga nyavu na nje na kubaki akilaumiwa na wenzake.

Yanga ilipata bao la kwanza dakika ya 18, lililowekwa wavuni na Mzize, aliyeruka juu na kuunganisha kwa kichwa mpira wa kona uliopigwa na Pacome Zouzoua.

Bao hilo liliwafanya wachezaji wa Yanga wawe kama wametiwa ufunguo, kwa sababu waliendelea kuliandama kwa kasi lango la Dodoma Jiji ambao walionekana kuchanganyikiwa na kufanya makosa mengi yaliyowatia matatani muda mwingi wa mchezo huo.

Haikushangaza waliposababisha penalti ambapo kipa wake, Mohamed Hussein, alipolazimika kutoka langoni kwenda kukabiliana na Dube kutokana na uzembe wa mabeki wake, lakini alimfanyia madhambi na mwamuzi, Ahmed Arajiga, kutoka Manyara 'akafunika'. Penalti hiyo ilitiwa ndani ya kamba na Aziz Ki dakika ya 28 ya mchezo.

Alikuwa ni Mzize kwa mara nyingine tena alipopachika bao la tatu dakika ya 37 kwa shuti la mbali, baada ya kuona lango lipo tupu.

Kosa lililiofanywa na mmoja wa mabeki wa Dodoma Jiji kutoa pasi nyuma, badala ya kuwapasia wenzake ilionekana kwenda kwa Pacome, hivyo kipa, Hussein alilazimika tena kwenda kuokoa, lakini hakupata msaada kwa mabeki wake, Yanga wakaupora mpira na kabla hajarejea, Mzize aliupiga kwa mbali na kukwama wavuni.

Kipindi cha pili kila timu ilifanya mabadiliko ambayo kwa kiasi fulani yaliisaidia Dodoma Jiji kutokana na kuonekana wanaonana, huku Yanga ikipunguza kasi yake iliyoanza nayo kipindi cha kwanza.

Ni kipindi ambapo Dube alipopachika bao la nne kwenye mchezo huo, dakika ya 62 lililotokana na makosa ya wachezaji wa Dodoma Jiji walipojaribu kupasiana karibu ya eneo la hatari, lakini walinyang'nywa na Aziz Ki aliyepiga shuti lililookolewa na kipa, mpira haukwenda mbali badala yake ulizua kizaazaa langoni kabla ya Dube kuukwamisha wavuni.

Dodoma Jiji imebaki na pointi 16, ikiwa nafasi ya 11, ikiwa imemaliza mechi zake 15 za mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu.

## Fadlu awaita nyota Simba ni Mashujaa, Kibu hauzwi ng'o

**Faustine Feliciane na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Simba, amewasifia wachezaji wake akisema wana tabia za kishujaa kwa sababu hawakati tamaa na wamejijengea tabia ya kucheza kwa kupambana mpaka filimbi ya mwisho, ameweka wazi kwa sasa, nyota wake, Kibu Denis, hauzwi.

Taarifa zilizopatikana jijini, Dar es Salaam jana zinasema Kibu, ambaye yuko Marekani kwa ruhusa maalumu anawindwa na Amazulu ya Afrika Kusini.

"Tayari klabu hiyo imeshafanya mazungumzo ya awali na Simba, lakini Fadlu ameweka wazi anamhitaji mchezaji huyo, yuko katika mipango yake," chanzo hicho kilisema.

Akizungumza baada ya mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya JKT Tanzania kumalizika juzi, Fadlu, alisema wachezaji wake wamekuwa na tabia ya kujituma na kucheza kwa malengo ya kusaka ushindi mpaka pale watakaposikia filimbi ya kumaliza mechi imelia huku akiwataka wanachama na mashabiki kuwa na moyo kama wao.

Kocha huyo alisema wachezaji wake wamekuwa na moyo wa kishujaa, kwa kuendelea kufanya mashambulizi makali licha ya ugumu wanaopata kutoka kwa wapinzani kwa lengo la kusaka ushindi hadi dakika za mwisho.

"Wachezaji wangu wameonesha fikra za kutokata tamaa, wanacheza kama mashujaa, wanapambana na kutokata tamaa hata kama dakika zinaelekea kumalizika, hata mashabiki wetu sasa wanapaswa kuwa na utamaduni kama wa wachezaji wao, kutokata tamaa hadi mwisho, hiki ndicho ninachotengeneza kwenye timu, angalia mechi kama tatu tunazimaliza kwa kupata ushindi mwishoni, dhidi ya Mashujaa, CS Sfaxien na leo (juzi)," alisema Fadlu.

Kuhusu mechi hiyo ya juzi ambayo walipata bao la jioni, Fadlu, raia wa Afrika Kusini aliisifu safu ya ulinzi ya JKT Tanzania ilikuwa ngumu kupitika, na Maafande hao walicheza zaidi nyuma na kushambulia kwa kushtukiza, hivyo kuwapa wakati mgumu.

Beki wa kati ya Simba, Abdulrazack Hamza, alieleza wazi walichokikuta uwanjani ni tofauti na kile walichotarajia.

Alisema ushindi huo umesaidia kuongeza pointi tatu na pia ugumu waliopata umewakumbusha timu sasa hivi zimejipanga sana hivyo wawe waangalifu.

Matokeo hayo yameifanya Simba kufikisha pointi 37 na kuendelea kujiimarisha kileleni huku JKT Tanzania ikiwa nafasi ya nane na pointi zake 19 kibindoni.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >